JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KWA MWAKA, 2024

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]

Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole,
S.L.P 941,
41105 **DODOMA**

6 FEBRUARI, 2025

YALIYOMO

YALIYOMO i

SEHEMU YA KWANZA 1

1.0 MAELEZO YA JUMLA 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Muundo wa Taarifa 1
1.3 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati 1
1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika 3

SEHEMU YA PILI 4

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA 4
2.1 Maelezo ya Shughuli 4
2.1.1 Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati 4
2.1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 5
2.1.3 Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge 6
2.1.4 Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa ... 11
2.1.5 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji 11
2.2 Uchambuzi wa Matokeo ya Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati 12
2.2.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Viwanda na Biashara 12
2.2.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Kilimo ... 28
2.2.3 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi 53

SEHEMU YA TATU 71

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO 71
3.1 Mtazamo na Maoni ya Jumla 71
3.2 Mapendekezo 74
3.2.1 Upungufu wa Mitaji na Bajeti ya Maendeleo kwa Taasisi na Mashirika ya Umma 74
3.2.2 Ukosefu wa Soko la Uhakika la Bidhaa Zinazozalishwa Nchini 74
3.2.3 Mfumo wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) 75

3.2.4 Hali ya mafuta ya kula nchini 76
3.2.5 Upatikanaji wa Sukari Nchini 77
3.2.6 Mkataba wa Ununuzi wa Viuadudu kati ya NDC na TAMISEMI 77
3.2.7 Upungufu wa Scanners Katika Mipaka Nchini 78
3.2.8 Sekta ya Biashara Nchini 78
3.2.9 Ujenzi wa Viwanda Nchini 79
3.2.10 Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (Ward *Agricultural Resources Centres*) 79
3.2.11 Mchango mdogo wa Tasnia ya Umwagiliaji katika Sekta ya Kilimo 80
3.2.12 Tasnia ya Chai Nchini 81
3.2.13 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) 82
3.2.14 Mfuko wa Pembejeo za Kilimo 82
3.2.15 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) 83
3.2.16 Chanjo ya Mifugo 84
3.2.17 Majosho na malisho ya mifugo 84
3.2.18 Uvuvi wa Vizimba 85
3.2.19 Udhibiti wa Uvuvi Haramu 85
3.2.20 Taasisi za Utafiti 85
4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA 87
4.1Hitimisho 87
4.2Hoja 89

SEHEMU YA KWANZA
1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa Kipindi cha Kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Taarifa hii inahusu shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha mwaka mmoja.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imeundwa na sehemu tatu kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi na maelezo ya shughuli za Kamati, Muundo wa Taarifa, msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

(ii) Sehemu ya pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;

(iii) Sehemu ya tatu inahusu maoni ya jumla, mapendekezo, hitimisho na kutoa hoja.

1.3 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati unatokana na Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inaeleza kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi wake. Aidha, Ibara ya 63(2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ina wajibu wa kufanya masuala mbalimbali yaliyoainishwa katika Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo ni: -

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
(iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na
(iv) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo: -
(i) Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;
(ii) Kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara inazozisimamia;
(iii) Kushughulikia Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka, 2024;
(iv) Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025 za Wizara inazozisimamia;
(v) Kujadili taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Desemba, 2024); na

(vi) Kufuatilia Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Mwezi Februari, 2024.

1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 142 ambayo pamoja na mambo mengine inataka kubainisha njia au mbinu zilizotumika; naomba kulijulisha Bunge kuwa Kamati ilitumia njia na mbinu zifuatazo: -

(i) Kufanya vikao na Wizara inazozisimamia kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo na Taasisi zake;

(ii) Kufanya ziara kwa lengo la kuona hali halisi ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara na Taasisi zake;

(iii) Kupokea, kujadili na kufanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali, ikiwemo taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Kushiriki mafunzo na semina mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taasisi Binafsi na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii; na

(v) Kufanya majumuisho ya masuala yaliyobainika katika vikao wakati wa majadiliano ili kuorodhesha mambo muhimu ya kutolewa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Spika, lengo la kutumia mbinu hizi mbalimbali ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kupata ufahamu wa kutosha katika maeneo wanayoyasimamia na kuishauri Serikali. Naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili Taarifa hii kwa kuzingatia ufanisi wa njia na mbinu zilizotumika.

SEHEMU YA PILI
2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

2.1 Maelezo ya Shughuli

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, Kamati hii ni miongoni mwa Kamati kumi na moja za kisekta inayosimamia shughuli za umma kwenye sekta tatu: Sekta ya Viwanda na Biashara, Sekta ya Kilimo na Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kwa mpangilio wa Wizara, Sekta hizo zipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi mtawalia.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha masharti ya Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanazingatiwa, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

2.1.1 Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia Bajeti za Wizara zilizo chini yake. Kwa msingi huo, tarehe 21 hadi 23 Machi, 2024, Kamati ilichambua bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (a) - (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Matokeo ya uchambuzi huo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 29 Aprili, 13 Mei na 22 Mei, 2024, wakati wa vikao vya Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti za Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 bado zipo katika hatua za utekelezaji wake, naomba kulijulisha Bunge kuwa ufuatiliaji wa bajeti hizo unaendelea na kwamba maoni na ushauri kuhusu utekelezaji utatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (5) ya Kanuni za Bunge.

2.1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 hadi 19 Machi, 2024 Kamati ilitembelea na kukagua jumla ya miradi nane (8) iliyotekelezwa na Wizara hizi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Miradi hiyo ni:-

(i) Mradi wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC);
(ii) Mradi wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) – Kilimanjaro Machine Tools (KMTC) ;
(iii) Mradi wa Ujenzi wa Minada ya Awali 10, Upili 4 na Mpakani 2 - Horohoro, Tanga;
(iv) Mradi wa Ukarabati wa Ghala la Kipawa – Dar Es Salaam;
(v) Mradi wa Jengo la Utawala la Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO);
(vi) Mradi wa Shirika la Uvuvi – TAFICO;
(vii) Mradi wa Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo (*Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation* – TEMDO); na
(viii) Mradi wa Shamba la Mbegu na Malisho la Vikuge – Kibaha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa, Miradi hiyo ikitekelezwa kwa ufanisi, itasaidia kuboresha maisha ya Watanzania na kuongeza ustawi wa wananchi na lengo kuu la Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakuwa limefanikishwa. Aidha, ahadi zilizotolewa kwa wananchi katika aya za 37, 40 na 49 za Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 zitakuwa zimetimizwa.

Mheshimiwa Spika, Masharti ya Kifungu cha 7(1) (d) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 6(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, nayo yalizingatiwa. Kamati ilitembelea mikoa tisa (9) ya Njombe, Dar Es Salaam, Morogoro, Tanga, Arusha, Kilimanjaro,

Tabora, Pwani, Iringa na Mbeya. Ziara hizo ziliwezesha Kamati kufuatilia masuala yafuatayo: -

(i) Utendaji wa Shirika la Viwango (TBS) katika eneo la Bandari ili kuona namna linavyotekeleza majukumu yake katika kuhakikisha linadhibiti ubora;

(ii) Kutembelea Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (*Ward Agricultural Resource Centres*) ili kuona utekelezaji wa uhaulishaji wa teknolojia na maarifa mbalimbali kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, wanaushirika na wadau mbalimbali wa kilimo na mifugo;

(iii) Kutembelea Kituo cha pamoja cha Mpakani Horohoro (*Horohoro One Stop Center*) - Tanga ili kuona upatikanaji wa huduma katika dirisha moja;

(iv) Kutembelea na kuona shughuli za kiwanda cha uzalishaji wa Sukari cha Bagamoyo Mkoani Pwani.

(v) Kuona mashamba ya mfano yaliyounganishwa kwenye Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unaoratibiwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB).

2.1.3 Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

Mheshimiwa Spika, ili kulisaidia Bunge kufuatilia maazimio yake, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka 2024 ya Shughuli za Kamati hii. Naomba kulijulisha Bunge kuwa, uchambuzi huo ulionesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio hayo. Hatua hizo zinajumuisha maazimio yaliyotekelezwa kikamilifu na yale ambayo yapo

katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake. Mchanganuo wa hatua za utekelezaji ni kama ifuatavyo: -

(a) **Sekta ya Viwanda na Biashara**

Mheshimiwa Spika, Bunge lilitoa Maazimio matano (5) kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2024. Taarifa ya utekelezaji imeonesha kuwa Maazimio yote yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mfano azimio kuhusu Vituo vya Pamoja vya Mipakani (OSBP) kukosa mashine za ukaguzi limeanza kutekelezwa kwa kufunga mashine katika Mpaka wa Tunduma/Nakonde. Pamoja na hatua hizi, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka na za makusudi ili kuhakikisha inajenga mifumo imara ya udhibiti wa uingizaji wa bidhaa nchini katika maeneo yote ya mipakani ikiwa ni pamoja na kufunga mashine za ukaguzi (*scanners*).

Vile vile azimio kuhusu Upungufu wa Viuatilifu Nchini limeanza kutekelezwa ambapo Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, imewezesha ujenzi wa Kiwanda cha Plant Biodefenders Ltd kilichopo Mkoani Kilimanjaro, chenye uwezo wa kuzalisha lita 20,000 kwa mwezi, sawa na acre pack 160,000 za viuatilifu aina ya VURUGA BIOCIDES. Viuatilifu hivi vinaweza kunyunyizia ekari 160,000 kudhibiti visumbufu mbalimbali kama wadudu mafuta, meal bugs na viwavi wa vitumba (*ballworms*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuisimamia vyema Sekta hii kwa kununua *scanner* itakayosaidia ukaguzi wa mizigo inayoingia na kutoka nchini. Hatua

hii itaongeza Pato la Taifa na kupunguza bughudha kwa wafanyabiashara ya kutumia muda mrefu kukaguliwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwa vituo vyote vya mipakani vifungwe *Scanners*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, uliipatia Kamati hii jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Serikali kuhusu utatuzi wa changamoto ya Mikopo ya Matrekta ya Kampuni ya URSUS na kuripoti kwenye taarifa ya mwaka pamoja na taarifa za bajeti. Maelekezo hayo yalitokana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu maoni na ushauri wa namna ya kutatua changamoto zinazowakabili wakulima waliokopa matrekta ya Kampuni ya URSUS iliyowasilishwa Bungeni tarehe 4 Septemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa za Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio hayo. Kamati ilichambua taarifa hiyo na kubaini yafuatayo:-

(i) Timu ya wataalam ya kufanya tathmini ya mikopo ya matrekta hayo iliundwa na kukamilisha kazi yake. Taarifa pia inaeleza kuwa kwa sasa Serikali inaendelea kuchakata taarifa hiyo kwa hatua mbalimbali; na
(ii) Maandalizi ya ndani ya kufanya ziara nchini Poland kwa lengo la kufanya majadiliano ya kidiplomasia yanaendelea

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hatua hizo ambazo zimechukuliwa na Serikali, Kamati pia ilifahamishwa kuwa Serikali imesimamisha zoezi la kukusanya madeni yatokanayo na mikopo hiyo ya matrekta na hivyo kupunguza kero kwa wananchi/wakulima waliokopa makrekta.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua hizo ambazo zimeanza kuchukuliwa na Serikali. Aidha, Kamati

inaitaka Serikali kukamilisha hatua zilizobaki ili kumaliza changamoto zilizoambatana na mikopo hiyo.

(b) **Sekta ya Kilimo**

Mheshimiwa Spika, Maazimio ya Bunge kuhusu Shughuli za Sekta hii yalikuwa tisa (9). Naomba kutoa taarifa kwamba, utekelezaji wa maazimio hayo kwa kiasi kikubwa unaendelea. Kwa mfano, Azimio lililohusu changamoto za kiuendeshaji za Kampuni ya Mbolea (TFC) zinazotokana na mfumo wa ununuzi katika Sekta za Umma. Taarifa ya utekelezaji ilieleza kuwa, Serikali kupitia Msajili wa Hazina (TR) na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeridhia TFC kuandaa utaratibu wa kununua mbolea na pembejeo nyingine moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

Azimio lililohusu Serikali kuweka mikakati ya kuanzisha viwanda vya mbolea nchini ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa mbolea, Kamati ilielezwa kuwa, Serikali imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya vya mbolea nchini ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2024 kuna viwanda viwili (2) vya ITRACOM – Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha tani zaidi ya 600,000 kwa mwaka na kiwanda cha Minjingu chenye uwezo wa kuzalisha tani 100,000 kwa mwaka.

Aidha, azimio lililohusu upungufu wa sukari nchini, Kamati ilijulishwa kwamba hatua mbalimbali zilichukuliwa katika kuhakikisha sukari inapatikana nchi nzima na kwa bei inayohimilika. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kuidhinisha uagizaji wa tani 410,000 katika kipindi cha miezi kumi na mbili (12), kuanzia Januari, 2024 hadi Desemba, 2024;

(ii) Kusimamia usambazaji wa sukari kila Mkoa na kuhakikisha inawafikia wananchi; na

(iii) Kutoa amri ya bei elekezi kupitia Tangazo la Serikali (*Government Notice - GN*) Na. 40A na 40B la tarehe 23 Januari, 2024 ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu waliopandisha bei kiholela wanashusha bei ya sukari na kuchukua hatua za kisheria kwa wale walioendelea kuuza tofauti na bei elekezi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi hizo za kukabiliana na uhaba wa sukari uliokuwa umejitokeza.

(c) **Sekta ya Mifugo na Uvuvi**

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, kuna jumla ya masuala manne (4) yaliyoguswa na maazimio ya Bunge. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa, maazimio yote manne (4) yapo kwenye hatua tofauti za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Azimio linalohusu malalamiko ya wananchi hasa wavuvi kulazimishwa kutumia vizimba ilihali wao hawaoni umuhimu huo kutokana na kukosa uelewa wa jambo hilo. Kamati ilifahamishwa kuwa, Wizara imetoa elimu kwa wadau 1,497 kati ya 6,493 waliokusudiwa. Suala hili ni endelevu hivyo Kamati inaihimiza Serikali kuendelea kuwafikia wadau wengi zaidi ili kuondoa changamoto zinazotokana na uelewa mdogo.

Vilevile Kamati ilijulishwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikifanya mapitio ya mara kwa mara kwenye Kanuni zake kwa lengo la kuunganisha, kupunguza na kuondoa baadhi ya tozo zisizo rafiki kwa lengo la kuboresha huduma kwa wavuvi na wadau wa uvuvi.

Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali ikamilishe mchakato huo mapema ili kuondoa tozo ambazo siyo rafiki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Kamati haijaridhishwa na mchakato wa uanzishwaji wa Mamlaka za Usimamizi wa Shughuli za Maendeleo za Sekta ya Mifugo pamoja na Sekta ya Uvuvi. Kamati inaitaka Serikali kuona umuhimu wa kukamilisha sehemu iliyobaki ili mamlaka hizi zianzishwe ziweze kutekeleza majukumu yake na kupata tija iliyokusudiwa kwenye Sekta husika.

2.1.4 Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 108 (1)** ikisomwa pamoja na kifungu **cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati ilishughulikia **Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 (*The Fair Competition [Amendment] Bill, 2024*).** Matokeo ya shughuli hiyo ni Maoni na Ushauri wa Kamati yaliyowasilishwa Bungeni tarehe 3 Septemba, 2024 wakati wa Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

2.1.5 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za taasisi ishirini na tano zilizo chini ya Wizara inazozisimamia. Lengo lilikuwa ni kufuatilia shughuli za umma chini ya taasisi hizo na kujiridhisha iwapo zinasaidia katika lengo la kuwezesha maisha bora kwa kila Mtanzania na ustawi wa watu kwa ujumla. Uchambuzi wa taarifa hizo ulifanyika kwa kuoanisha maudhui, hali halisi na matarajio ya wananchi katika Sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, utaratibu wa kupokea na kujadili taarifa kutoka Serikalini uliiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa

Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, bado upo umuhimu wa kuzisisitiza Wizara ziendelee kutoa taarifa za kina na zenye takwimu sahihi zinazohitajika kwenye Kamati za Bunge kwa wakati ili kutimiza dhana ya uwazi na uwajibikaji Bungeni. Iwapo Taarifa zitawasilishwa kwa kuchelewa zitawanyima Wajumbe fursa ya kufanya uchambuzi wa kina na kuathiri tija ya uchambuzi.

2.2 Uchambuzi wa Matokeo ya Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea shughuli hizo, sehemu hii ya Taarifa inaonesha uchambuzi wa kina wa yaliyojitokeza na kubainisha ubora na dosari. Lengo ni kuhakikisha kuwa shughuli za umma zilizotekelezwa katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii zinazingatia matarajio ya wananchi. Naomba kulijulisha Bunge matokeo ya uhakiki yanayoonesha mafanikio na changamoto kwa kila Sekta kama ifuatavyo: -

2.2.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Viwanda na Biashara

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda na Biashara ni chimbuko la maendeleo ya haraka ya nchi mbalimbali. Sekta hii imekuwa mhimili mkuu wa kutegemewa kwa ajili ya kuongeza thamani ya malighafi, kutoa ajira kwa wananchi, kuongeza mapato ya Serikali pamoja na fedha za kigeni. Aidha, Sekta hii huongeza na kuboresha sayansi na teknolojia ambayo kwa pamoja huongeza ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa umeonesha mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Viwanda na Biashara kwenye Miradi na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

(a) **Baraza la Ushindani Tanzania (*Fair Competition Tribunal - FCT*)**

Mheshimiwa Spika, Baraza la Ushindani ni Mamlaka ya Rufaa iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Mamlaka hii ilianzishwa na Serikali chini ya kifungu cha 83(1) cha Sheria ya Ushindani Namba 8 ya Mwaka 2003 (*Fair Competition Act, No. 8/2003*) sura ya 285. Sheria hii ilianza kutumika Mwaka, 2004 baada ya Waziri mwenye dhamana kutangaza katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003, jukumu kuu la Baraza la Ushindani (*Fair Competition Tribunal*) ni kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri yote ya rufaa yatokanayo na ushindani wa kibiashara na udhibiti wa Soko kutoka vyombo mbalimbali. Vyombo hivyo ni pamoja na EWURA, TCRA, LATRA, TCAA na FCC pamoja na Taasisi zote ambazo Sheria zao zimeelekeza rufaa za mashauri kuletwa kwenye Baraza hili (FCT).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifahamishwa kuhusu mafanikio ya Baraza kama ifuatavyo: -

(i) Usajili na usikilizwaji wa Mashauri ambapo kuanzia Aprili, 2021 hadi Julai, 2024 Baraza lilipokea jumla ya mashauri 80; kati ya hayo, mashauri 64 yamekwishatolewa maamuzi sawa na asilimia 80 na mashauri 16 yanaendelea katika hatua mbalimbali za usikilizwaji;

(ii) Baraza limefanya Mapitio ya Kanuni za Baraza (*Tribunal Rules, 2012*) kwa hatua mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa mashauri ambapo mapitio hayo yalikuwa yanasubiri upitishwaji wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani ili Kanuni hizo zihuishwe kabla ya kuendelea na hatua za mwisho;

(iii) Katika kipindi cha miaka mitatu, Baraza limeendelea kuhakikisha shughuli zake zinafahamika vyema kwa umma na makundi mbalimbali katika jamii kama vile Wakulima na Wafanyabishara/Wawekezaji, Watoa huduma, Watumishi wa Umma na Walaji. Baraza hili limetoa Elimu kupitia Maonesho ya Saba Saba; Nane Nane; Siku ya Ushindani Duniani; Wiki ya Sheria; Siku ya Mlaji Duniani; na Wiki ya Utumishi wa Umma;

(iv) Baraza limeendelea kufanya Tafiti za kiuchumi na kisheria katika sekta za maji, nishati, mawasiliano, usafiri na ushindani wa kibiashara na kuwezesha kutoa ushauri wa kitaalam; na

(v) Mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza yameendelea kutolewa ambapo katika kipindi chote Wajumbe wa Baraza katika nyakati tofauti baada ya uteuzi wamehudhuria mafunzo maalum ya kina juu ya Sheria mbalimbali zinazotumika katika kuendesha mashauri kwenye Baraza.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya Baraza la Ushindani Tanzania, Kamati ilifahamishwa kuwa, Baraza linakabiliwa na changamoto ya Bajeti ndogo na upungufu wa watumishi wa kutekeleza shughuli za msingi kama vile utafiti wa kisheria na kiuchumi katika ushindani na udhibiti; uelimishaji kwa wadau na jamii juu ya shughuli za Baraza na haki katika ushindani wa Soko. Hali hii pia imeathiri uwepo wa mafunzo ya kutosha kwa Watumishi na Wajumbe wa Baraza.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iongeze bajeti ya kutosha kwa Baraza ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(b) **Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO)**

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) lilianzishwa na Sheria ya Bunge Na. 28 ya mwaka 1973 ikiwa ni utekelezaji wa AGIZO la Kamati Kuu ya Chama cha TANU la mwezi Machi, 1973 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2023. SIDO ilianzishwa ili kuiwezesha Serikali kujenga msingi mzuri wa kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo nchini.

Majukumu mahsusi ya SIDO ni pamoja na:-

(i) Kutoa huduma za maendeleo ya kiteknolojia na kiufundi, kwa ajili ya matumizi ya viwanda vidogo na vya kati;
(ii) Kuendeleza ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya chini ya programu ya kiatamizi;
(iii) Kutoa mafunzo na huduma za ugani;
(iv) Ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wajasiriamali;
(v) Kuwezesha bidhaa za viwanda vidogo kuyafikia masoko; na
(vi) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati.

Mheshimiwa Spika, SIDO katika kutekeleza majukumu yake, imepata mafanikio yafuatayo kwa kipindi cha miaka mitatu 2020/2021 hadi 2023/2024:-

(i) Kutoa huduma za kiufundi na maendeleo ya Teknolojia kwa viwanda vidogo na vya kati;
(ii) Kuendeleza ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya chini ya programu ya kiatamizi;
(iii) Kutoa mafunzo na huduma za ugani;
(iv) Ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya wanaviwanda;
(v) Kuwezesha bidhaa za viwanda vidogo kuyafikia masoko; na
(vi) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyotajwa, Kamati ilibaini pia changamoto zinazoikabili SIDO kama ifuatavyo:-

(i) Kutokuwa na vyanzo vya mapato vya kudumu na endelevu ambapo fedha zinazotengwa na Serikali ni kiasi kidogo hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuzingatia kuwa, uhitaji wa huduma za SIDO umekuwa ukiongezeka kutokana na hamasa ya Wananchi ya uongezaji wa thamani wa malighafi na jitihada za Serikali za uhamasishaji ukuaji na uanzishaji wa viwanda;

(ii) Shirika lina madeni ya Ardhi kiasi cha **Shilingi 4,045,427,569** yanayotokana na tozo za kibiashara katika maeneo yake badala ya tozo za huduma. Hali hiyo imesababisha kuwa na limbikizo la madeni kwa kuwa maeneo hayo yanatumika kuvilea Viwanda Vidogo kwa kuvipatia maeneo ya kufanyia kazi kwa tozo ya gharama nafuu.

(iii) Shirika lina upungufu wa Watumishi 179 ili kuwezesha kutoa huduma kwa wananchi ipasavyo. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Shirika limendelea kutumia Watumishi wa ajira za mikataba pamoja na wahitimu wa kujitolea huku taratibu za kuomba ajira za kudumu zikiendelea; na

(iv) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya mitaa ya viwanda iliyojengwa miaka ya 1980 ni changamoto. Vilevile, ukosefu wa magari unakwamisha kuwafikia walengwa, hivyo kupunguza kasi ya maendeleo ya viwanda vidogo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi ulionesha kwamba, kukosekana kwa vyanzo vya mapato vya kudumu na endelevu kunakwamisha jitihada za SIDO kusaidia vijana na wanawake kujikwamua na wimbi la umaskini.

Kamati inaishauri Serikali kuiongezea fedha SIDO iweze kufanya ukarabati; na vile vile ipelekewe watumishi wa kutosha ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake na kuleta tija iliyokusudiwa.

(c) **Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO)**

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) ilianzishwa na Serikali kwa Sheria ya Bunge Namba 23 ya Mwaka 1980 ili kujenga uwezo katika kubuni, kusanifu, kuunda mitambo na mashine, kuhamasisha utengenezaji wa mashine na mitambo, kutoa huduma za kihandisi viwandani na kutoa mafunzo kwa mafundi na wahandisi walioko viwandani ili kuongeza tija na weledi.

Mheshimiwa Spika, TEMDO inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria kama ifuatavyo:-

(i) Kutafiti, kubuni, kuendeleza na kuunda mitambo, mashine na vifaa pamoja na teknolojia mbalimbali. Majukumu mengine ni kuhamasisha utengenezaji wake kibiashara na matumizi yake katika shughuli za uzalishaji mali ili kukuza uchumi;

(ii) Kutoa huduma za kihandisi kwenye viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kwa lengo la kuongeza ufanisi, matumizi bora ya rasilimali, ubora wa bidhaa na uwezo wa ushindani;

(iii) Huduma za maendeleo ya kiteknolojia na kiufundi, kwa ajili ya matumizi ya viwanda vidogo na vya kati; na

(iv) Kutoa mafunzo kwa wahandisi na mafundi mchundo wanaofanya kazi viwandani na Taasisi zingine ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha miaka mitatu (3), TEMDO imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Kusanifu na kutengeneza Jokofu la ngazi sita la kuhifadhia maiti;

(ii) Kutengeneza mtambo wa kukausha mazao ya kilimo kwa kuanzia na zao la muhogo. Mtambo huu umekamilika kwa asilimia 100 na majaribio yalifanyika kwenye karakana ya TEMDO kwa ushirikiano na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB);

(iii) Mtambo wa kuchoma taka hatarishi za hospitalini ambao unatumia dizeli unawezesha kuchoma taka za hospitali kwa ukamilifu bila kuleta madhara mengine kwa nyuzi joto 800^0C – 1400^0C;

(iv) Kutengeneza mashine za kukamulia mbegu za alizeti zenye kiwango bora. Pia inasanifu na kutengeneza mitambo ya bei nafuu ya kuchuja mafuta ya alizeti kwa ajili ya wajasiriamali wenye mtaji wa kati. Vilevile, TEMDO imebuni na kutengeneza mtambo wa kukamua na kusindika michikichi; na

(v) TEMDO imeunda na kufanya majaribio ya teknolojia ya kutengeneza mkaa unaotokana na vumbi la mbao pamoja na mkaa unaotokana na mabaki ya mimea kama vile jatropha, maganda ya karanga, pamoja na pumba za mpunga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa, TEMDO inakumbana na changamoto katika utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Ufinyu wa bajeti ya maendeleo ambapo TEMDO imekuwa ikiidhinishiwa kiwango kidogo cha fedha za maendeleo kulingana na mahitaji yake halisi;

(ii) Ukosefu wa masoko ya uhakika ya vifaa tiba na bidhaa zingine zinazozalishwa na TEMDO hivyo kuathiri mapato ya Taasisi. Wizara ya Afya kupitia MSD hawanunui bidhaa zinazozalishwa na TEMDO; na

(iii) Upungufu wa Wafanyakazi ambapo Taasisi ina wafanyakazi 86 ukilinganisha na mahitaji ya wafanyakazi 128, hivyo bado kuna upungufu wa wafanyakazi 42.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ikipewa umuhimu unaostahili inaweza kupunguza gharama za kuagiza baadhi ya vifaa ikiwemo mitambo mbalimbali ambayo inaagizwa nje ya nchi wakati inaweza kuzalishwa na TEMDO. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea TEMDO fedha za Miradi ya Maendeleo pamoja na watumishi. Aidha, Serikali iweke utaratibu wa kununua bidhaa/vifaa vinavyotengenezwa na TEMDO vyenye ubora kwa kuipa upendeleo maalum ili kuipa Taasisi soko la uhakika ikiwa ni pamoja na kuipunguzia Serikali gharama.

(d) **Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilianzishwa mwaka 1975 kwa Sheria ya Viwango Sura 130 na kuanza kazi rasmi tarehe 16 Aprili, 1976 ambapo pamoja na majukumu mengine, lilipewa jukumu la kuratibu uandaaji wa viwango na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake TBS imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Katika kipindi cha miaka mitatu 2021/2022 – 2023/2024 Shirika limefanikiwa kutayarisha na kufanyia mapitio viwango kwa asilimia 97.7 ambapo viwango 1,730 viliandaliwa ikilinganishwa na lengo la kuandaa viwango 1,770;

(ii) Shirika kwa kutumia wakala linakagua magari yaliyotumika (*used motor vehicles*) kabla ya kuingia nchini kupitia kampuni mbili za ukaguzi wa magari ambazo ni EAA Company Ltd inayokagua magari nchini Japan na Uingereza (UK) na Quality Inspection Services Japan - QISJ inayokagua magari Dubai iliyopo katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE);

(iii) Shirika hupima ubora wa bidhaa kwa kupitia sampuli zinazoletwa kwenye maabara za TBS. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024, jumla ya sampuli 99,051 sawa na asilimia 97.1 ya lengo la kupima sampuli 102,000 zilipimwa katika maabara kwa lengo la kuhakiki ubora;

(iv) Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024, jumla ya vifaa 31,628 vilifanyiwa ugezi sawa na asilimia 100.4 ya lengo la kufanyia ugezi vifaa 31,500;

(v) Shirika limeendelea kutoa elimu kwa wazalishaji wa bidhaa za viwandani, wasindikaji na umma wote wa Watanzania kuhusu dhana nzima ya viwango vya ubora na usalama wa bidhaa; na

(vi) Shirika linafanya huduma ya kusajili bidhaa za chakula na vipodozi kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuhakiki ubora wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa katika utekelezaji wa majukumu yake, TBS inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Uwepo wa njia zisizo rasmi za kuingiza bidhaa kutoka nje ya nchi, jambo ambalo linapelekea uwepo wa bidhaa hafifu sokoni;

(ii) Wajasiriamali wadogo kushindwa kuvuka kipindi cha uangalizi cha miaka mitatu (3) na hivyo kushindwa kuchangia gharama za uthibiti kwa mujibu wa utaratibu uliopo kwa sasa;

(iii) Baadhi ya wafanyabiashara wasio waadilifu hususan waingizaji wa mizigo hapa nchini wanaotumia utaratibu wa kutoa mizigo bandarini kukiuka masharti na kusababisha kuongezeka kwa bidhaa zisizo na ubora hapa nchini; na

(iv) Watumishi kutopandishwa mishahara kwa zaidi ya miaka 12 wakati gharama za maisha zimeendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha utendaji wa Shirika hili kwa kulipatia vitendea kazi ikiwemo rasilimali watu na fedha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa TBS hasa mishahara, mafunzo ya mara kwa mara na kuwapa motisha ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi na weledi.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara ili kuongeza uadilifu katika kufanya biashara na kuboresha mifumo na miundombinu ya udhibiti wa bidhaa kwa lengo la kulinda ubora na usalama wa watumiaji.

(e) **Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala - WRRB**

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala *(WRRB)* ni Taasisi iliyoundwa kwa Sheria Namba 10 ya mwaka 2005 na Marekebisho Kifungu 4 Sura 339 R.E. 2016. Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ulianzishwa kwa dhumuni la kukuza juhudi za Serikali kurasimisha mifumo ya masoko iliyopo kwa lengo la kupunguza vikwazo vya uzalishaji wenye tija na utafutaji masoko kwa bidhaa mbalimbali hususan mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Bodi katika utekelezaji wa majukumu yake imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Mapato ya mkulima na ya Serikali yameongezeka kwa wastani wa asilimia 38 kutokana na urasimishaji;

(ii) Kuchochea ubora wa mazao yanayofikishwa sokoni;

(iii) Upatikanaji wa takwimu sahihi za mazao yanayopita kwenye Mfumo wa Stakabadhi za Ghala; na

(iv) Kukuza huduma za fedha vijijini na kufanikisha uanzishaji wa Soko la Bidhaa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana Bodi inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Upinzani mkubwa toka kwa wafanyabiashara na wadau wengine wanaonufaika na mifumo isiyo rasmi ambapo hununua kwa bei ndogo na vipimo visivyo rasmi kutoka kwa wakulima;

(ii) Wakulima kuwa na uelewa mdogo wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

(iii) Maagizo kinzani na Sheria ya Stakabadhi za Ghala wakati wa utekelezaji wa Mfumo;

(iv) Wadau saidizi kama vile Vyama Vikuu vya Ushirika kuchelewesha malipo kwa wakulima licha ya fedha kulipwa kwa wakati katika akaunti zao;

(v) Uhaba wa maghala bora na ya kisasa; na

(vi) Ufinyu wa bajeti ya Bodi na kusababisha uhaba wa vitendea kazi kama magari na vifaa vya mifumo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, Mfumo huu wa Stakabadhi za Ghala ni mzuri kwa kuwa unaweka utaratibu unaowawezesha wazalisha bidhaa kukusanya nafaka katika Ghala Kuu kwa malengo mbalimbali. Miongoni mwa malengo hayo ni kuuza kwa pamoja kupitia minada ya upili kwa lengo la kupata bei nzuri; kupata huduma za kifedha kama vile mikopo; na kuhifadhi ghalani ili kurahisisha usindikaji.

Mheshimiwa Spika, Mtazamo wa Kamati ni kuwa, ili malengo mazuri ya uanzishwaji wa mfumo yafikiwe, Serikali haina budi kuongeza nguvu katika kukabiliana na changamoto zilizopo, hasa kwa kuwekeza kwenye utoaji wa elimu kwa wakulima na wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu na manufaa ya Stakabadhi za Ghala. Kwa msingi huo, Kamati inaona kuna umuhimu kwa Serikali kuiongezea bajeti Bodi hii iweze kufikia malengo ya kuwa na maghala bora na vitendea kazi vingine ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

(f) **Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)**

Mheshimiwa Spika, majukumu ya CAMARTEC yapo kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 19 ya 1981.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu cha utekelezaji wa majukumu yake, CAMARTEC imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Kubuni, kuunda na kufanya majaribio ya kiutendaji ya teknolojia mbalimbali zinazorahisisha kazi na kuondoa shuruba kwa wakulima na wafugaji nchini;

(ii) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa vijana na kueneza teknolojia za nishati mbadala kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia, kuhifadhi misitu na mazingira na kukuza kipato na ajira;

(iii) Kushirikisha Sekta zisizo Rasmi katika uzalishaji wa teknolojia na huduma nyingine kwa kutumia Wataalam na Karakana ya CAMARTEC kwa lengo la kukuza ajira na kipato;

(iv) Kufanya majaribio ya zana za kilimo na teknolojia za Vijijini kwa lengo la kuwalinda wananchi na Taifa dhidi ya zana za kilimo ambazo hazina ubora na zisizofaa kwa matumizi nchini; na

(v) Serikali kupitia CAMARTEC imeandaa Mkakati wa Mawasiliano kwa Umma, Mkakati unaolenga kutangaza na kutoa elimu kwa Umma juu ya shughuli mbalimbali za Taasisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, CAMARTEC inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Ufinyu wa bajeti kulingana na mahitaji na shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa fedha husika. Fedha zinazotengwa hazitoshi kufanya ununuzi wa mashine mpya na za kisasa kwa ajili ya karakana ili kujenga uwezo wa kufanya utafiti; ujenzi wa maabara na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya majaribio ya zana za kilimo na teknolojia za vijijini;

(ii) Upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali ambapo kwa sasa Kituo kina watumishi 77 tu kati ya 171 wanaoihitajika;

(iii) Uwezo mdogo wa kununua (*Low Purchasing Power*) wa Wadau wa teknolojia za CAMARTEC ambapo Wadau wakubwa wa teknolojia za CAMARTEC ni wakulima waishio vijijini. Aidha, wengi wao hawana uwezo mkubwa wa kumudu kununua zana za kilimo na teknolojia za vijijini zinazobuniwa na kutengenezwa na CAMARTEC; na

(iv) CAMARTEC haina eneo la kufanyia majaribio ya kitaalam ya vifaa vinavyotengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi changamoto nyingi zinazoikabili CAMARTEC zinatokana na ufinyu wa bajeti. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga na kuipatia taasisi hii fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, uwezo mdogo wa kununua wa wateja wa bidhaa za CAMARTEC unaweza kutatuliwa kwa kuipatia taasisi hii ruzuku na hivyo kuuza bidhaa zake kwa bei nafuu. Serikali inashauriwa kuipatia Taasisi hii eneo la kufanya majaribio.

(g) **Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)**

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) lilianzishwa kwa Hati ya Serikali ya Uanzishwaji wa NDC kupitia Tangazo la Serikali Na. 90 la Mwaka 1969 (*The National Development Corporation (Establishment) Order, G.N. No. 90 of 1969)*.

Majukumu ya Shirika yamebainishwa katika sheria hii pamoja na uamuzi wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 1996 (*Cabinet Paper No.* 6/96). Shirika hili limeendelea

kuwepo chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura Na. 257 ya mwaka 2002. Jukumu kubwa la Shirika ni kuendeleza na kutekeleza miradi ya kimkakati kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake Shirika la Maendeleo la Taifa limepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Kusaini Mkataba wa Uchimbaji Madini ya Chuma Maganga Matitu na Kampuni ya Fujian Hexingwang Industry Tanzania Co. Ltd. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 2 Agosti, 2024 Mkoani Njombe;

(ii) Kufanya uthamini wa fidia za mali za wananchi wa Maganga Matitu ambapo **Shilingi Milioni 536** zimetumika kulipa wanaopisha Mradi wa Makaa ya Mawe Katewaka na Chuma Ghafi Maganga Matitu;

(iii) Kufufua Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools (KMTC) ambacho kimeanza uzalishaji baada ya kusimama kwa zaidi ya miaka 36;

(iv) Kuendeleza miundombinu kwenye Kongani la TAMCO ikiwemo kukamilika kwa ujenzi wa mita 230 za barabara kwa kiwango cha lami; na

(v) Kuendeleza mashamba ya mpira ya Kihuhwi na Kalunga na hivyo kuchangia malighafi ya mpira kwenye viwanda nchini. Baadhi ya viwanda vinavyotumia mpira unaozalishwa na NDC ni kiwanda cha viatu cha Bora (*Bora Shoes*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa, NDC inakabiliana na changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa majukumu yake ya msingi. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na: -

(i) Sheria iliyoanzisha NDC ni ya muda mrefu na hivyo inahitaji kufanyiwa mapitio kwa lengo la kuiboresha ili kwenda na wakati;

(ii) Wakati Shirika lina wajibu wa kuhodhi ardhi na leseni za madini kwa niaba ya Serikali (kama mwendelezaji na mtunzaji) kwa matumizi ya sasa na kizazi kijacho, Shirika linalazimika kulipa kiasi kikubwa cha fedha kama kodi ya ardhi na ada ya leseni za madini;

(iii) Sehemu ilipo miradi ya kimkakati ikiwemo ya Mchuchuma, Liganga, Engaruka na Kongani za Viwanda hakuna miundombinu ya barabara, maji na umeme;

(iv) Kukosekana kwa mfumo madhubuti wa maandalizi ya miradi kumesababisha Shirika kukosa miradi yenye sifa inayohitajika (*Bankable Projects*). Hivyo, kutegemea wawekezaji kufanya maandalizi ya miradi ikiwemo tafiti za kiasi, ubora na aina ya madini;

(v) Shirika linakabiliwa na uhaba wa watumishi wenye utaalam na ujuzi wa kutekeleza majukumu yake;

(vi) Shirika linakabiliwa na changamoto ya Mtaji mdogo ikilinganishwa na majukumu yake uliosababishwa na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Ubinafsishaji huo uliiondolea mtaji NDC pamoja na kampuni zilizokuwa zinaleta faida kwa Shirika. Jumla ya mali zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 40 ziliondolewa kwenye Shirika; na

(vii) Shirika lilikabidhiwa maeneo na viwanda vyenye madeni makubwa ya kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazolikabili Shirika hili zinaweza kutatuliwa iwapo Serikali italipa umuhimu unaostahili ikiwa ni pamoja na kupeleka miundombinu katika miradi ya kimkakati ili kuimarisha mazingira na kuvutia wawekezaji. Aidha, upungufu wa mtaji pamoja na uhaba wa wataalam na watumishi wenye ujuzi utatuliwe ili shirika liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itoe kipaumbele katika kutatua changamoto za Shirika ili kupata tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia katika uchambuzi wake, imebaini uwepo wa changamoto kubwa inayosababishwa na kutotekelezwa kwa Mkataba wa Ununuzi wa Viuadudu kati ya NDC na TAMISEMI uliopelekea deni la mtaji wa uendeshaji wa Kiwanda cha Viuadudu la NSSF kuongezeka kutokana na riba. Kamati inaishauri Serikali kusimamia Taasisi zake na Halmashauri katika kutekeleza mkataba wa kununua viuatilifu kutoka Kiwanda cha Viuadudu Kibaha. Aidha, Kamati inashauri Kiwanda cha Viuadudu kipanue shughuli zake na kuzalisha viuadudu vya mazao ya kilimo.

2.2.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, maendeleo katika Sekta ya Kilimo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa sekta ya viwanda. Ukuaji wa sekta hii una umuhimu mkubwa katika kuzalisha chakula cha kutosha ili kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula na lishe kwa wananchi wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kujadili na kuchambua taarifa mbalimbali za Wizara ya Kilimo kuhusu

utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zinazoikabili Sekta ya Kilimo nchini kama ifuatavyo: -

(a) **Utendaji wa Taasisi ya Mafunzo ya Kilimo, MATI – Mtwara**

Mheshimiwa Spika, MATI - Mtwara ni miongoni mwa vyuo kumi na tatu (13) vinavyosimamiwa na Wizara ya Kilimo. Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Kilimo Mtwara (MATI-Mtwara) ulianza Februari, 1974 chini ya ufadhili wa *International Development Agency-IDA 3rd Project*. Lengo likiwa ni kuwa na taasisi ya kutoa mafunzo ya taaluma ya kilimo na mifugo, ambapo mafunzo rasmi yalianza kutolewa Juni, 1975.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, MATI - Mtwara imepata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Tangu kuanzishwa kwa Chuo mwaka 1975, jumla ya wanafunzi 4,393 wamehitimu mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya astashahada ya kilimo. Idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa imeongezeka kutoka 40 waliodahiliwa mwaka 1975 na kufikia 357 kati ya mwaka wa masomo 2019/20 na 2023/24;

(ii) Matumizi ya Mtaala Uliohuishwa Kupitia Programu ya ASDP II ambao ulipelekea kuanzishwa kwa mtaala wa Agriculture Production. Hivyo, kuanzia mwaka wa masomo 2019/20, Chuo kilianza utekelezaji wa mtaala huo ambapo kilisajili wanafunzi 367. Mwaka 2020/21, Chuo kilisajili wanafunzi 329; mwaka 2021/22, wanafunzi 362; na mwaka 2022/23 wanafunzi 365;

(iii) Kuendelea na Programu ya Mafunzo ya Kilimo Biashara kwa Vijana 1,710 iliyoanza tarehe 20

Machi, 2023, ambayo ni sehemu ya Programu ya Jenga kesho iliyo bora ili kuongeza ushiriki wa vijana kwenye sekta ya kilimo;

(iv) Chuo kimekuwa kikishirikiana na wadau pamoja na mashirika mbalimbali kama vile Japan International Cooperation Agency (JICA), Lindi and Mtwara Agribusiness Support Project (LIMAS), Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), Catholic Relief Service (CRS), Bodi ya Korosho na Halmashauri za Lindi na Liwale ambapo kati ya mwaka 2019 na 2023 kimefanikiwa kutoa mafunzo kwa wakulima 4,189 kutoka katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma;

(v) Kukarabati na Kuboresha Miundombinu katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 ambapo Chuo kilipokea Shilingi 1,517,495,083.00 kwa ajili ya ukarabati wa maeneo ya miundombinu yanayohusisha wanafunzi kujifunzia ambayo ni madarasa, maabara, maktaba, jengo la utawala, bwalo, jiko, ujenzi wa vyoo, darasa la wakulima, mabweni, ujenzi wa power house na kujenga mtandao wa ardhini wa umeme;

(vi) Serikali imekipatia Chuo matrekta mawili (2) na zana zake kwa ajili ya huduma za mafunzo pamoja na uzalishaji ili kiweze kujitegemea;

(vii) Chuo kimeendelea kupanda na kupanua Shamba la kuzalisha korosho, kupanda miche 359,496,055 ya matunda na miti kwa ajili ya mafunzo, uzalishaji na utunzaji wa mazingira;

(viii) Mwaka wa fedha 2019/2020, Chuo kilingia makubaliano na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) ya kuzalisha mbegu bora za mazao ya ufuta na mahindi. Katika mwaka huo, Chuo kilizalisha mbegu bora za ufuta tani 3.9 na mwaka 2020/21

tani 11.7 za mbegu bora ya ufuta. Aidha, kuanzia mwaka 2022/23 Chuo kilitakiwa kuzalisha mbegu bora za mahindi, ambapo kilizalisha tani 42.5 na mwaka 2023/24 kilizalisha tani 59.1 za mbegu bora ya mahindi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, MATI – Mtwara inakabiliwa na changamoto ambazo zinahitaji ufumbuzi ili kuleta ufanisi.

(i) Chuo kina uhaba wa watumishi hali inayopelekea ugumu katika kutekeleza majukumu yake; na

(ii) Uvamizi wa ardhi ya chuo unaofanywa na wananchi wanaozunguka kutokana na kukosekana kwa Hati Miliki.

Mheshimiwa Spika, chuo hiki kimekuwa na manufaa mengi kwa jamii ya wakulima na kilimo nchini. Changamoto zinazokikabili kama vile uvamizi wa ardhi ya chuo unaofanywa na wananchi unasababisha kuibuka kwa mgogoro baina ya chuo na wananchi hao kutokana na kutokuwepo kwa hati miliki ya ardhi ya chuo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kukamilisha mchakato wa kukipatia hati miliki ya ardhi chuo hicho pamoja na kuweka mipaka katika eneo lote. Aidha, zoezi hili lifanyike kwa vyuo vyote vya kilimo vyenye changamoto kama hii.

Vilevile, majukumu ya chuo hiki bado hayajafahamika sana kwa wananchi na hivyo kutotumika kikamilifu ikiwa ni pamoja na kutopata wanafunzi wa kutosha na wakulima kutonufaika na huduma zinazotolewa na chuo hiki. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kukitangaza kupitia vyombo mbalimbali vya Habari

ikiwemo luninga (television), redio na mitandao ya kijamii.

(b) **Utendaji wa Bodi ya Sukari (SBT)**

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Sukari Tanzania inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Tasnia ya Sukari Na.26 ya Mwaka 2001 Sura ya 251. Kifungu hicho kimeainisha majukumu makuu ya Bodi ya Sukari Tanzania ambayo ni pamoja na:-

(i) Kutoa huduma za udhibiti;
(ii) Kusimamia na kuratibu maendeleo ya tasnia ya sukari nchini;
(iii) Kuendeleza mafunzo na tafiti za kukuza ujuzi katika tasnia ya sukari nchini;
(iv) Kuendeleza teknolojia katika tasnia ya sukari nchini; na
(v) Kusimamia uzalishaji, usambazaji na biashara ya sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa Bodi katika kutekeleza **majukumu** yake imepata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Kuongezeka uzalishaji wa sukari katika kipindi cha miaka kumi (2012/2013-2022/2023) iliyopita kutoka tani 299,698 hadi tani 460,048.94 sawa na asilimia 53.5 ya uzalishaji;

(ii) Utambuzi wa maeneo mapya yanayofaa uwekezaji wa miradi mipya ya sukari na kuandaa ramani ya maeneo hayo ambapo maeneo ya Songea, Rufiji na Kasulu yameshapata wawekezaji;

(iii) Kuendeleza Teknolojia katika Tasnia ya Sukari kwa kushirikiana na Taasisi ya TEMDO, kutekeleza mradi wa ujenzi wa kiwanda kidogo cha sukari cha kuzalisha tani 4,000 hadi 5,000 kwa mwaka;

(iv) Kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa kusajili wakulima na mashamba yao kwa kushirikiana na Dar Teknohama Business Incubator (DTBi); na

(v) Kuongeza tija ya uzalishaji kwa mashamba ya wakulima wadogo kutoka wastani wa Tani 42.92 kwa hekta hadi Tani 55.32 kwa hekta ndani ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya makubwa, Kamati imebaini kuwa Bodi ya Sukari Tanzania inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaweza kupunguza kasi ya uzalishaji wa Sukari nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni hizi zifuatazo:-

(i) Kukosekana kwa mikopo ya muda mrefu kutoka Taasisi za Fedha yenye riba ndogo na masharti nafuu;

(ii) Kutokuwepo kwa "*products diversification*" katika viwanda vya sukari nchini;

(iii) Tija ndogo ya mashamba ya miwa hasa ya wakulima wadogo;

(iv) Ukosefu wa miundombinu ya barabara za mashambani na ya umwagiliaji katika mashamba ya wakulima wadogo;

(v) Ukosefu wa mbegu bora zinazostahimili magonjwa, wadudu na ukame;

(vi) Mlipuko wa ugonjwa wa vidung'ata wa njano ambao haukuwepo hapo awali katika Kanda ya Afrika Mashariki;

(vii) Mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha mvua kubwa kupita kiasi au ukame au milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu ambao hapo awali hawakuwepo;

(viii) Uwepo wa wafanyabiashara wanaoingiza sukari kwa njia za magendo hususan katika mikoa ya pembezoni; na

(ix) Ukosefu wa sukari ya viwandani inayohitajika sana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mikakati ya kuhakikisha sukari ya kutosha inazalishwa hapa nchini ili kupunguza kutegemea kutoka nje ya nchi na vilevile kuzalisha bidhaa zaidi ya moja yaani sukari, umeme na methanol. Hivyo basi, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kutatua changamoto hizo kama vile ya kukosekana kwa mikopo ya muda mrefu kutoka Taasisi za Fedha yenye riba ndogo na masharti nafuu;

Aidha, Serikali ihakikishe kuwa miundombinu ya barabara za mashambani na ya umwagiliaji katika mashamba ya miwa ya wakulima wadogo inatengenezwa ili kurahisisha usafirishaji. Kamati inashauri uwekezaji ufanyike ili uzalishaji wa sukari ya viwandani ufanyike hapa nchini.

(c) **Utendaji wa Bodi ya Kahawa (TCB)**

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Kahawa Tanzania (*Tanzania Coffee Boad – TCB*) ni Taasisi ya Umma iliyoundwa chini ya Sheria ya Bunge Na. 23 ya Mwaka 2001 (*The Coffee Industry Act, CAP. 347*) na Marekebisho yake ya Sheria za Mazao Na. 20 ya Mwaka 2009 (*The Crop Laws Miscellaneous Amendments Act*).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Bodi ya Kahawa Tanzania imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa miche bora ya kahawa ambapo Bodi iliweka lengo la kuzalisha miche milioni 20 kila mwaka katika mpango mkakati wake wa 2020 – 2025. Kwa mwaka wa fedha 2023/24 jumla ya miche 22,628,919 ilizalishwa sawa na asilimia 113.1 ya malengo;

(ii) Katika kipindi cha miaka minne cha utekelezaji wa mpango mkakati, zao la kahawa limeingiza fedha za kigeni kiasi cha Dola za Marekani 791,105,867 sawa na zaidi ya Shilingi trillion mbili za Kitanzania. Fedha hizi zimetokana na mauzo ya kahawa nje ya nchi;

(iii) Kuongezeka kwa wastani wa bei ya mkulima ambapo bei anayopata mkulima wa kahawa imeendelea kuimarika kutoka wastani wa Shilingi 2,200 kwa kilo ya kahawa ya robusta ya maganda msimu wa 2022/2023 hadi wastani wa Shilingi 5,000 kwa msimu wa 2024/2025;

(iv) Kupungua kwa kahawa za magendo na biashara zisizo rasmi hasa kwa kahawa iliyokuwa inazalishwa mikoa ya mipakani hususani Mkoa wa Kagera iliyokuwa ikitoroshwa kwenda nchi jirani. Bodi ya Kahawa imeboresha mazingira ya biashara yaliyowezesha kuimarika kwa bei na kupunguza gharama za kufanya biashara;

(v) Kuongeza ujuzi katika Tasnia ya Kahawa ambapo Bodi ya Kahawa ndio Taasisi pekee yenye kuendesha kozi ya kahawa kwa ngazi ya cheti kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi. Kozi

hiyo inaitwa Cheti cha Ubora wa Kahawa na Biashara (*Certificate in Coffee Quality and Trade*) ya mwaka mmoja iliyoanzishwa ili kuziba pengo la wataalamu wa ubora wa kahawa, biashara na wagani wa kahawa na pia imeondoa utegemezi wa wataalam wa aina hii kutoka nchi za jirani; na

(vi) Bodi imefanikiwa kusogeza huduma kwa wadau wa kahawa katika maeneo ya uzalishaji wa kahawa kwa kufungua ofisi za kanda katika mikoa mitano (5) ya Ruvuma (Mbinga), Mbeya, Kagera, Mara (Tarime) na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Tasnia ya Kahawa nchini inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kubadilishwa kwa matumizi ya ardhi ya kilimo cha kahawa hususani katika mikoa ya Kaskazini (Kilimanjaro na Arusha) kwa ajili ya makazi au kwa shughuli nyingine za Kilimo na Utalii hivyo kusababisha kushuka kwa uzalishaji katika mikoa hiyo;

(ii) Mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha kupungua kwa maji kwa ajili ya umwagiliaji na mtawanyiko mbaya wa mvua na vipindi virefu vya ukame katika maeneo yanayolima kahawa;

(iii) Matumizi duni ya pembejeo hususan mbolea za viwandani kwa wakulima wadogo yanasababisha tija ndogo na tofauti kubwa ya uzalishaji kati ya msimu hadi msimu; na

(iv) Utegemezi wa soko la nje kwa zaidi ya asilimia 90 na kukua kwa kasi ndogo kwa soko la ndani la kahawa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake za kurejesha tija katika Tasnia ya Kahawa nchini. Aidha, changamoto kama riba kubwa ya mkopo wa pembejeo inayofika asilimia 17, inapelekea matumizi duni ya pembejeo na hivyo kupunguza tija. Kamati inashauri changamoto hizi ziwekewe mikakati ya kuziondoa ili wakulima wapate faida na kuongeza mwamko kwa wakulima wengi zaidi kuwekeza kwenye kilimo cha kahawa. Kuboreshwa kwa mazingira ya kahawa kutaondoa pia changamoto ya kubadilishwa kwa matumizi ya ardhi ya kilimo cha kahawa hususani katika mikoa ya Kaskazini (Kilimanjaro na Arusha).

Kamati inaishauri Serikali kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kilimo cha Kahawa nchini na kuyawekea utaratibu mzuri. Vilevile, Kamati inashauri kuwa wakati sasa umefika zao la kahawa liingizwe kwenye mfumo wa stakabadhi za ghala na pia Taasisi ya Utafiti wa zao la kahawa iendelee ili kuongeza ufanisi kwenye eneo la utafiti.

(d) **Bodi ya Chai (TBT)**

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Chai Tanzania (*Tea Board of Tanzania - TBT*) ni Taasisi ya Umma iliyo chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 3(1) Sheria ya Tasnia ya Chai Na. 3 ya Mwaka 1997 na kuanza rasmi shughuli zake tarehe 1 Oktoba, 1997.

Sheria hii pia ilianzisha Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania. Sambamba na uwepo wa taasisi hizi, TBT imekuwa ikitekeleza shughuli zake kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania inayoendeshwa kupitia ubia wa sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa katika utekelezaji wa majukumu, Bodi ilipata mafanikio yafuatayo: -

(i) Imefanikiwa kuanzisha mnada wa chai jijini Dar es Salaam ambao huendeshwa kila Siku ya Jumatatu kupitia Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa njia ya kieletroniki. Mnada huu umewezesha sehemu ya chai inayozalishwa Tanzania kuuzwa katika soko hilo badala ya kutegemea Soko la Mombasa;

(ii) Kuanzishwa kwa kiwanda cha chai maalum cha Sakare ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Chai Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni ya Kazi Yetu Ltd imewezesha wakulima wa chai katika Wilaya ya Korogwe kupitia chama cha msingi cha ushirika wa wakulima wadogo wa chai Sakare (Sakare Amcos);

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Kamati ilifahamishwa kuhusu uwepo wa changamoto mbalimbali zinazoikabili Tasnia ya Chai nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni hizi zifuatazo:-

(i) Madeni ya wakulima wadogo wa chai kutokana na kushuka kwa mauzo ya chai kavu kwenye soko la dunia. Hali hii imesababisha baadhi ya viwanda kushindwa kulipa wakulima wadogo wa majani mabichi ya chai kwa muda muafaka kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Chai; na hivyo kusababisha uzalishaji wa chai kupungua nchini hasa kwenye maeneo ya wakulima wadogo, ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2024, jumla ya madai ya wakulima yalikuwa Shilingi 2,768,340,221. Aidha, tatizo la madeni na kudorora kwa tasnia ya chai limechangiwa na uwepo wa wawekezaji (mfano, DL Holdings Ltd na Mohamed Enteprises), wanaomiliki viwanda na mashamba ya chai ambayo kutokana na uwezo mdogo wa kimtaji na migogoro ya kibiashara hayazalishi;

(ii) Tija ndogo na uzalishaji wa chai ambapo uzalishaji wa chai kwa wakulima wadogo ni wastani wa kilo 950 kwa hekta kwa mwaka na wakulima wakubwa ni wastani wa kilo 1,200 kwa hekta kwa mwaka;

(iii) Gharama kubwa za uzalishaji na uendeshaji wa mitambo ya chai hususani umeme na umwagiliaji ambapo suala hili limechangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa uzalishaji kutokana na uwezo mdogo wa wadau kumudu gharama hizi;

(iv) Hali duni ya miundombinu (Barabara na Umeme) kwenye maeneo yanayolima chai hasa kipindi cha masika inaathiri usafirishaji wa majani mabichi ya chai kutoka kwa wakulima wadogo kwenda viwandani na chai kavu kutoka viwandani kwenda sokoni. Hali hii imesababisha wastani wa zaidi ya tani 5 za chai za majani mabichi kupotea kutokana na miundombinu ya barabara kutopitika hasa kipindi cha masika ambacho uzalishaji wa chai unakuwa juu (*peak season*); na

(v) Mabadiliko ya tabia nchi yameathiri uzalishaji kwenye maeneo mengi yanayolima zao la chai hapa nchini na kusababisha kuwa na kipindi kirefu cha kiangazi ambacho kimeathiri uzalishaji wa chai kwenye maeneo yanayolima chai.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zinahitaji ufumbuzi wa kudumu ili kuimarisha zao la chai nchini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kulisimamia zao hili kwa karibu ikiwa ni pamoja na kushughulikia wawekezaji ambao wameshindwa kuendeleza zao la chai na hivyo kudhoofisha wakulima wa chai.

Aidha, Serikali iweke utaratibu wa kutoa taarifa za mara kwa mara kwa wakulima wa chai kuhusu mwenendo wa bei katika soko la dunia pamoja na kukaa na wenye viwanda waliosimamisha uzalishaji wa zao la chai ili kufufua viwanda vyao au kuwapa/kuwauzia wawekezaji wenye uwezo. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, ili kuwa na tija kwenye zao la chai, Serikali ihakikishe Miradi ya Umwagiliaji inaelekezwa kwenye maeneo ya mashamba ya chai ya wakulima wadogo na wa kati.

(e) **Mfuko wa Pembejeo za Kilimo - AGTF**

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ulianzishwa mwaka 1994 chini ya Kifungu cha Tatu (3) cha Sheria ya Mfuko wa Pembejeo, [Sura ya 401] pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa pembejeo una majukumu yafuatayo:-

(i) Utoaji wa mikopo ambapo tangu Mfuko uanzishwe, mikopo 3,985 yenye thamani ya shilingi 94,726,458,665 imetolewa ikiwemo mikopo ya trekta ambayo inachangia asilimia zaidi ya 51 ya mikopo yote;

(ii) Utoaji wa mikopo kwa vijana kupitia Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) ambapo dirisha la kupokea maombi ya mikopo kutoka kwa vijana na wanawake kupitia Programu ya "Jenga Kesho Iliyo Bora" (BBT-YIA) lilifunguliwa tarehe 30 Aprili, 2023. Hadi kufikia Desemba, 2024, maombi 1,546 yenye thamani ya shilingi bilioni 21.3 yamepokelewa

(iii) Urejeshaji wa mikopo kwa kipindi cha 2021/2022 – 2024/25 ambapo hadi kufikia nusu ya mwaka 2024/2025, hali ya urejeshwaji wa mikopo haikuwa

ya kuridhisha kutokana na changamoto ya kuwa na mikopo chechefu ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoukabili Mfuko wa Pembejeo ambazo ni hizi zifuatazo:-

(i) Wingi wa mikopo chechefu ya muda mrefu;

(ii) Ucheleweshwaji wa fedha kutoka Hazina;

(iii) Upungufu wa watumishi; na

(iv) Umbali kati ya mkopaji na mkopeshaji ambao unaongeza gharama za ukaguzi na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mfuko unaimarika na kuboresha utendaji wake kwa kuweka mikakati ya kukusanya mikopo chechefu ikiwa ni pamoja na kufuta kwenye vitabu mikopo iliyoridhiwa na ya muda mrefu. Aidha, malengo ya Serikali ya kuwawezesha wakulima wadogo hasa vijana na wanawake yanafikiwa kwa kuwawezesha kupata mikopo yenye riba nafuu ambayo itawawezesha kujiongezea kipato na kuboresha maisha yao na hatimaye kuongeza uchangiaji katika Sekta ya Kilimo nchini.

(f) **Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*Cereals and Other Produce Board - CPB*)**

Mheshimiwa Spika, CPB ilianzishwa kwa Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Namba 19 ya mwaka 2009 (*The Cereals and Other Produce Act No.19 of 2009*) ikiwa na jukumu la kufanya biashara ya nafaka na mazao mengine ili kuwawezesha wakulima kupata soko la uhakika na bei shindani ya mazao yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 CPB imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Kupunguza utegemezi Serikalini kutoka asilimia 3.7 kwa mwaka 2022/2023 hadi asilimia 2.4 mwaka 2023/2024 na inaendelea kupungua kwani katika kipindi cha nusu mwaka wa 2024/2025 Bodi haijapokea fedha yoyote kutoka Serikalini;

(ii) Kupanua masoko kwa kufanya biashara na Mashirika ya Kimataifa ikiwemo Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) ambalo hununua mazao kama mahindi na kusafirisha katika nchi mbalimbali; katika kipindi cha nusu mwaka wa 2024/2025 Bodi ilipata USD 2,700,000 kutokana na mauzo ya mahindi kiasi cha tani 7,500 kwa WFP; na

(iii) Kuongeza wigo wa mapato kutoka kuuza mazao na nafaka hadi kutoa huduma ya usagishaji wa nafaka kwa wadau mbalimbali pamoja na kukodisha ghala. Kwa sasa CPB inatoa huduma ya usagishaji wa mahindi kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na huduma ya usagishaji wa unga wa ngano kwa Kampuni ya EPIC Haulage Ltd. Katika kipindi cha nusu mwaka wa 2024/2025, Bodi imekusanya jumla ya Shilingi 288,522,084 kutokana na utoaji wa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Kamati ilibaini CPB inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinakwamisha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama ifuatavyo:-

(i) Mtaji usiotosheleza (*insufficient working capital*). Pamoja kwa kwamba CPB inapata kibali cha kukopa kutoka Serikalini, lakini bado inahitaji kuwa

na mtaji ili iweze kutumia kwa ufanisi mkopo unaopatikana kutoka katika mabenki ya kibiashara (overdraft);

(ii) Ajira zenye ukomo wa miaka miwili umepelekea Bodi kupoteza wafanyakazi wengi ambao wamekwisha jengewa uwezo. Hali hii inaathiri uendeshaji wa viwanda na miundombinu ya hifadhi;

(iii) Kutokuwa na ofisi katika Kanda ya Mashariki. Kanda ya Mashariki yenye makao yake makuu katika Mkoa wa Dar es Salaam haina ofisi za kudumu. Hali hii inasababisha utendaji wa ofisi hii kutokuwa wa kuridhisha;

(iv) Muundo wa CPB kutoendana na majukumu halisi ambayo inayatekeleza na dira iliyojiwekea;

(v) Mabadiliko ya mara kwa mara ya bei katika tasnia ya nafaka na bidhaa za viwandani yanasababisha Bodi kutokufanya biashara kiufanisi; na

(vi) CPB ilirithi miundombinu ya viwanda na ghala kutoka lililokuwa Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) ambayo ni chakavu na inahitaji ukarabati mkubwa na hivyo kuifanya CPB kutumia fedha nyingi kufanya ukarabati wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Bodi hii ni chombo muhimu katika kuweka uwiano kwenye tasnia ya nafaka na kumlinda mkulima dhidi ya bei kandamizi. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia CPB kwa ukaribu na kutatua changamoto zinazoikabili za kimuundo kwa kuifanya kampuni yenye uwezo na mtaji wa kushindana sokoni. Pia ijenge ofisi katika Kanda ya Mashariki yenye Makao yake Makuu Jijini Dar es Salaam.

Aidha, Serikali iajiri watumishi wa kudumu CPB badala ya hali ilivyo sasa ambapo kuna watumishi wenye ajira zenye ukomo wa miaka miwili. Hali inayopelekea Bodi kupoteza wafanyakazi ambao wamekwisha jengewa uwezo. Hii inaathiri uendeshaji wa viwanda na miundombinu ya hifadhi.

(g) **Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA)**

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249 kwa lengo la kusimamia na kudhibiti nafaka na mazao mchanganyiko kuanzia hatua ya uzalishaji, uchakataji, biashara na masoko.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, katika kutekeleza majukumu yake, mamlaka imepata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Kuanza kurasimisha mifumo ya usimamizi wa biashara ya mazao ya ufuta, mbaazi, dengu, kakao na soya inayochochea ushindani na inayoongeza kipato cha mkulima;

(ii) Kuweka bei kinga na kutumia mizani za kidijitali inayosaidia kupata uzito sahihi wa kilo kwa mazao yanayopita katika mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

(iii) Kusimamia upatikanaji wa bei inayoendana na soko la dunia kwa wakulima kwa mazao kama kakao, dengu, mbaazi, ufuta na soya ambapo mazao hayo yameuzwa nchini kwa takribani kati ya asilimia 70 hadi 101 ya bei ya kwenye soko la Dunia;

(iv) Kusajili wanunuzi wa nafaka na mazao mchanganyiko 170 katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo kati ya hao wanunuzi 145 (85%) wameshiriki minada ya kidijitali kwa msimu huu;

(v) Kuimarisha mifumo ya kupata takwimu sahihi za mauzo ya mazao;

(vi) Kufanikisha upatikanaji wa fedha kwa mkulima kwa mifumo rasmi na ufanisi ambapo katika msimu 2023/2024 wakulima wamelipwa jumla ya shilingi 751,036,705,157.00 kutokana na mauzo ya mazao ya ufuta, mbaazi, dengu na soya kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kidijitali katika mikoa tisa ya Songwe, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Singida, Dodoma na Manyara;

(vii) Katika kuhakikisha taasisi inatekeleza Agenda 10/30 "kilimo biashara", Mamlaka imeweka mazingira wezeshi ya kibiashara kitaifa na kimataifa kwa kufanikisha kutoa vibali vya kusafirisha nje ya nchi na kuingiza ndani ya nchi nafaka na mazao mchanganyiko; na

(viii) Mamlaka imeendelea kujitambulisha kwa wadau mbalimbali na kutoa elimu ya majukumu yake kupitia majukwaa mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii, vyombo vya habari, kushiriki kwenye mikutano ya wadau, pamoja na warsha na makongamano.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilielezwa kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana lakini zipo changamoto zinazoikabili Mamlaka hii katika utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Uelewa mdogo wa wadau kuhusu COPRA na majukumu yake;

(ii) Upungufu wa watumishi;

(iii) Kutokuwa na mifumo kwenye mikoa mingine ya Tanzania ambayo inazalisha mazao ambayo yamewekewa miongozo na kusababisha utoroshaji;

(iv) Uelewa mdogo wa Wakulima kuhusu matumizi ya mfumo wa ununuzi na uuzaji wa mazao;

(v) Ucheleweshwaji wa malipo kutoka kwenye chama kikuu kumfikia mkulima kwa baadhi ya minada; na

(vi) Fedha iliyoidhinishwa na Bunge ni finyu na haipatikani kwa wakati ambapo inasababisha COPRA kushindwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyopangwa kwenye Mpango na Bajeti pamoja na Sheria ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili COPRA zinaweza kutatuliwa ikiwa Serikali itaongeza bajeti ya kutosha kuiwezesha kupeleka mfumo kwenye maeneo yote yanayohitaji huduma hiyo ili kuondoa kabisa utoroshoshwaji wa nafaka na mazao mchanganyiko. Kamati pia inaishauri Serikali kuipatia COPRA watumishi wa kutosha kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Vilevile, Kamati inaitaka Serikali kuweka mazingira mazuri ya ujenzi wa maghala ya kutosha na kuhakikisha yanajengwa maeneo ambayo wakulima watayafikia kwa urahisi, badala ya ilivyo sasa wakulima wanasafirisha mazao umbali mrefu kwa gharama kubwa.

(h) **Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Sura 245.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa mafanikio ambayo wakala imepata katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula kwa tani 90,000 (Babati, Mpanda na Sumbawanga);

(ii) Kutoa ajira kwa wananchi 7,601, kati ya hao vijana walikuwa 4,326;

(iii) Kuwajengea uwezo wa kiteknolojia ya ujenzi na usanifu wa mifumo ya vihenge vya kisasa kwa makampuni ya wazawa;

(iv) Kuongeza fursa za kiuchumi kwa wananchi wa maeneo ya mradi kwa kutoa fursa za kibiashara;

(v) Kuboresha mandhari ya maeneo vihenge vilipojengwa; na

(vi) Watumishi walipewa mafunzo ndani na nje ya nchi juu ya uendeshaji wa vihenge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Kamati imebaini uwepo wa changamoto zifuatazo: -

(i) Kuchelewa kupatikana kwa suluhu ya Mkandarasi M/S Feerum S.A ambaye amevunja Mkataba isivyo halali na kupelekea mradi kusimama kwa maeneo ya Dodoma, Makambako, Songwe, Songea na Shinyanga;

(ii) Uhaba wa fedha za kununua chakula kwa ajili ya akiba ili kufikia malengo iliyojiwekea;

(iii) Uhaba wa watumishi, Wakala unakabiliwa na uhaba wa watumishi wa kutosha ili kutimiza majukumu yake ipasavyo; na

(iv) Baadhi ya wakulima kuleta nafaka zisizo na ubora kwenye vituo vya ununuzi wa nafaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua ya kuhifadhi sukari kupitia Wakala huu katika kukabiliana na upungufu wa sukari pindi unapojitokeza. Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kununua mazao ya nafaka kutoka kwa wakulima kwa wakati, pamoja na kusimamia ubora wa nafaka hizo kwenye vituo.

Suala la Mkandarasi M/S Feerum kutopata suluhu limeendelea kuwa kikwazo katika kutekeleza miradi kwenye maeneo yanayoguswa na mkataba wake. Kamati kwa mara nyingine tena inatoa rai kwa Serikali kupata suluhisho la Mkandarasi huyu ili kuruhusu kukamilisha miradi ambayo imesimama na kuokoa gharama zitokanazo na mradi kutokamilika kwa wakati. Elimu zaidi ya uhifadhi wa nafaka katika hatua zote itolewe ili kuwawezesha wakulima kupata mazao bora yatakayonunuliwa na Wakala bila kipingamizi.

(i) **Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (*Ward Agricultural Resource Centres - WARCs*)**

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Rasilimali za Kilimo vilianzishwa mwaka 2006/2007 kufuatia tathmini ya huduma za ugani katika Wizara za Sekta ya Kilimo (Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), ambayo ilionesha kuwepo kwa changamoto

ya uhaba wa Maafisa Ugani uliochangia kutofikiwa kwa wakulima na wafugaji na huduma za ushauri wa kitaalam. Jukumu la ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa vituo hivyo lilifanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Wizara ya Kilimo ilihusika kutoa mwongozo wa kuanzisha na kuendesha vituo hivyo pamoja na ramani ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Novemba, 2024, zilikuwepo jumla ya WARCs 278 kati ya 3,956 sawa na asilimia 7 zilizopo nchini. Kati ya vituo hivyo, 180 vinatumika, 39 vimebadilishiwa matumizi na 45 havijakamilika.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha vituo hivyo ni kuwa kitovu cha kuhaulisha teknolojia na maarifa mbalimbali kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, wanaushirika na wadau mbalimbali wa kilimo. Katika kufikia azma hiyo, malengo mahususi yaliwekwa kama ifuatavyo:-

(i) Watoa huduma za kilimo na mifugo wa Sekta ya Umma na Binafsi kutumia vituo hivyo kutoa huduma za kilimo;
(ii) Tafiti mbalimbali za kilimo, mifugo na uvuvi kufanyika katika vituo hivyo;
(iii) Kuweka mashamba darasa na ya mfano kwa ajili ya wakulima na wafugaji kujifunza;
(iv) Kuwa jukwaa la wadau wa kilimo kukutana na kujadili mafanikio, changamoto na kuweka mipango ya kuendeleza kilimo; na
(v) Sehemu ya kutolea mafunzo kwa wakulima na kupata huduma za kilimo ikiwemo pembejeo na zana.

Mheshimiwa Spika, Vituo hivyo vinakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Kubadilishiwa matumizi na kuwa nyumba za Makatibu Kata, Ofisi za Kata, stoo za kuhifadhia vyakula na shule za awali;
(ii) Havina Maafisa Ugani wa kutoa elimu kwa wananchi;
(iii) Havina vifaa vya kisasa kama computer na photocopy machines;
(iv) Kukosekana kwa miundombinu ya maji, umeme na barabara;
(v) Kukosa uzio; na
(vi) Baadhi kukosa hati miliki za ardhi na hivyo kusababisha migogoro isiyo ya lazima baina ya Serikali na Wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa Serikali iweke mkakati wa kuvifufua vituo hivi na kuvirudisha kwenye matumizi yaliyolengwa na kuviwekea usimamizi madhubuti ili tija ipatikane. Aidha, Serikali ikamilishe ununuzi wa matrekta na vifaa vingine ili vituo hivi vitakaporudishwa viwe ndiyo mechanization centres kwa ajili ya kutoa huduma za matrekta na zana nyingine kwa wakulima wa kawaida.

(j) **Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - NIRC**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa pamoja na kutembelea baadhi ya miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji chini ya Wizara ya Kilimo na kujionea namna ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya kuratibu, kuendeleza na kusimamia Maendeleo ya Sekta ya Umwagiliaji nchini, Tume katika Mwaka wa

Fedha 2023/2024 na 2024/2025 imefanikiwa kusimamia na kutekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Mradi wa kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW).

Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 150 ambapo Tume imetengewa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 13.3;

(ii) Miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika Bonde la Usangu na kuimarisha vyama vya umwagiliaji katika uendeshaji na matunzo ya miundombinu. Hadi 30 Septemba, 2024, ujenzi na ukarabati wa skimu za Mbuyuni Kimani yenye jumla ya hekta 3,200 na Makangarawe (hekta 1,200) umefikia asilimia 25; na

(iii) Ujenzi wa skimu ya Madibira (hekta 3200) umefikia asilimia 99 ya kazi zilizopangwa kwa mujibu wa mkataba;

(iv) Uchimbaji wa Visima kupitia Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Nchini (TFSRP-PFoR) unaogharimu dola za Marekani milioni 70 na kutarajiwa kuwa na *Co-Financing* kutoka JICA kwa gharama ya dola milioni 71. Katika mradi huu, jumla ya visima 67,000 vya umwagiliaji vimepangwa kuchimbwa kupitia ifikapo mwaka 2030 katika Halmashauri 184 nchini; na

(v) Utekelezaji wa Mradi wa Ushauri wa JICA (*JICA Irrigation Advisory Project*) ambao unaendelea kama ifuatavyo:-

- Ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za msingi za skimu za umwagiliaji 69 kupitia dodoso zimefanyika.

- Uchaguzi wa skimu 8 zitakazotumika katika mafunzo ya Mwongozo Kabambe wa Umwagiliaji kwa watumishi wapya wa Tume; na

(vi) Watumishi wa Makao Makuu pamoja na watumishi 56 kutoka mikoa 7 wamepatiwa Mafunzo ya Mwongozo kabambe wa Umwagiliaji katika Uibuaji, Utekelezaji, Uendeshaji na Matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita, kwa kuendelea kutenga fedha ambazo zimeanza kuleta mapinduzi katika kilimo cha umwagiliaji nchini ikiwa ni mpango wa kupunguza utegemezi wa kilimo cha kutegemea mvua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya makubwa, Kamati imebaini kuwa Tume inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazopunguza kasi ya utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni hizi zifuatazo: -

(i) Kuchelewa kwa fedha za utekelezaji wa bajeti kutoka Wizara ya Fedha;

(ii) Mwamko mdogo wa wakulima katika kulipa ada za huduma za umwagiliaji;

(iii) Mabadiliko ya tabianchi; changamoto ya mvua kubwa za *el-nino* imeathiri kasi ya utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji na kupelekea uharibifu wa kazi za ujenzi zilizokuwa zikiendelea katika baadhi

ya skimu ikiwemo Skimu za Rudewa (Kilosa) na Mkombozi (Iringa).

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe mtiririko wa upatikanaji wa fedha za umwagiliaji unazingatia muda na kiwango cha kuridhisha ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, kuna umuhimu wa Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kutatua changamoto kama vile ya wakulima kutolipa ada za huduma za maji kwa wakati ili kuendelea kuhudumia miundombinu ya umwagiliaji.

2.2.3 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi

(a) **Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)**

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Namba 29 ya Mwaka 1994. Kitengo kinasimamiwa na Bodi ya Wadhamini yenye jukumu la kusimamia, kudhibiti na kuongoza shughuli za uhifadhi katika maeneo yaliyotangazwa kuwa Hifadhi za Bahari (*Marine Parks*) na Maeneo Tengefu (*Marine Reserves*).

Mheshimiwa Spika, kitengo hiki kimepewa majukumu mahsusi yafuatayo:-

(i) Kuanzisha, kulinda na kuhifadhi maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa bioanuai pamoja na mifumo ikolojia ya baharini na mwambao wa pwani;

(ii) Kusimamia maeneo ya bahari na mwambao wa pwani ili kuwezesha matumizi endelevu ya rasilimali na kuhuisha maeneo yaliyoharibiwa;

(iii) Kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi wanashirikishwa ipasavyo katika

nyanja zote za upangaji, uendelezaji na usimamizi wa Hifadhi na Maeneo Tengefu, pia wanapata manufaa yatokanayo na Hifadhi na wanapewa kipaumbele katika matumizi ya rasilimali na fursa za kiuchumi zinazojitokeza;

(iv) Kuongeza uelewa kwa wadau na jamii juu ya mazingira na usambazaji wa taarifa kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali kwenye Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu;

(v) Kuhamasisha wananchi kutumia rasilimali ambazo hazitumiki kabisa au hazitumiki kikamilifu kwa sasa; na

(vi) Kuwezesha kufanyika kwa tafiti, ufuatiliaji na tathmini za hali ya matumizi ya rasilimali kwenye maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu tajwa, kitengo hiki kimepata mafanikio mengi ikiwemo haya yafuatayo:-

(i) Kuanzishwa kwa hifadhi tatu (3) na maeneo tengefu kumi na tano (15) kwenye bahari ya Hindi hivyo kusababisha uwepo wa shughuli endelevu za uvuvi kutokana na upatikanaji wa samaki;

(ii) Kuongezeka kwa mtandao wa matumbawe hai (ambayo ni mazalia muhimu ya samaki) yenye wastani wa juu kati 40% hadi 50% ikilinganishwa na wastani wa 25%;

(iii) Kuimarika kwa bioanuai na mifumo ya ikolojia ikiwemo kuongezeka kwa aina mbalimbali za samaki zilizo hatarini kutoweka. Mathalani, miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko la samaki aina ya Papa Potwe

kutoka 5 mwaka 2000 hadi 226 mwaka 2024 katika Hifadhi ya Bahari ya Mafia ambapo kimekuwa ni kivutio kikubwa cha utalii;

(iv) Kuimarika kwa bioanuai na mifumo ikolojia ikiwemo kuongezeka kwa aina mbalimbali za samaki zilizo hatarini kutoweka;

(v) Kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo Kitengo kimekuwa kikipata Hati safi;

(vi) Kuimarika kwa vivutio katika Maeneo ya Hifadhi za Bahari kutokana na kulindwa na kuhifadhiwa na hivyo kutoa fursa ya uwekezaji na shughuli za utalii wa kiikolojia.;

(vii) Kuimarika kwa mifumo ikolojia katika maeneo ya hifadhi inayochochea uendelevu wa mazao ya uvuvi; na

(viii) Kutengeneza na kuzindua Mpango wa Kitaifa wa Uhifadhi wa Kasa pamoja na kuandaa rasimu ya Mpango wa Kitaifa wa Uhifadhi na Ulinzi wa Matumbawe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, MPRU inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994 imepitwa na wakati na taratibu za kufanya mapitio zilianza tangu mwaka 2015;

(ii) Upungufu wa mtaji wa uhifadhi (*conservation capital*) na utalii ambapo MPRU imekuwa

ikitegemea mapato yanayotokana na shughuli za utalii katika maeneo yaliyohifadhiwa ambayo ni hafifu na hayatoshelezi;

(iii) Katika utekelezaji wa shughuli za utalii ili kupata mapato ya kujiendesha, MPRU imekuwa ikikumbana na ugumu kwa kutumia sheria ya utalii kitu ambacho kimekuwa kikisababisha mgongano wa kimaslahi; na

(iv) Uvamizi wa maeneo ya Hifadhi na matumizi ya zana haribifu zisizo endelevu katika uvuvi, kuongezeka kwa idadi ya watu, uhamiaji wa wavuvi na utegemezi mkubwa wa rasilimali za uvuvi kwa ajili ya kujikimu kwa wakazi wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizotajwa kuikabili MPRU zinaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa iwapo sheria inayosimamia kitengo hiki itafanyiwa mapitio kwa kuwa imepitwa na wakati. Aidha, iongeze bajeti ili kukuza mtaji kwenye kitengo hiki ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, Serikali iongeze kasi katika kudhibiti uvamizi na matumizi ya zana haribifu na zisizo endelevu katika uvuvi ili kupata tija iliyokusudiwa.

(b) **Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (*Tanzania Fisheries Research Institute - TAFIRI*)**

Mheshimiwa Spika, TAFIRI ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 6 ya Mwaka 1980 na kuhuishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 11 ya Mwaka 2016, kwa lengo la kufanya utafiti wa uvuvi na ukuzaji viumbe na kuishauri Serikali katika kuendeleza, kuimarisha na kulinda Sekta ya Uvuvi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza wa mjukumu yake, TAFIRI imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Katika kipindi cha mwaka 2023/2024, Taasisi imetekeleza jumla ya miradi ya utafiti 23 na imetoa machapisho (*publications*) 45 kwenye majarida ya kimataifa;

(ii) TAFIRI imefanya tathmini ya Kimkakati ya Mazingira (*Strategic Environmental Assessment*) ili kuainisha maeneo yanayofaa kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika Ziwa Victoria (Geita, Mara, Simiyu, Mwanza na Kagera);

(iii) TAFIRI Kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ilifanya utafiti wa ikolojia na uvuvi na kubaini uwepo wa aina 846 za samaki ambapo utafiti ulibaini aina mpya 10 kwenye maji ya Tanzania;

(iv) TAFIRI inaendelea na ujenzi wa atamizi maalum inayolenga kuweka miundombinu ya kuzalisha mbegu na chakula bora cha samaki katika Ziwa Victoria; na

(v) TAFIRI imetekeleza kazi ya ujenzi wa vivutia samaki (*FADs*) 10 ambavyo vitawekwa baharini ili kuongeza mavuno ya samaki hasa kwa wavuvi wadogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, TAFIRI inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa meli za kutosha kwa ajili ya kufanyia utafiti. Kwa sasa Taasisi ina meli mbili tu ambapo moja ipo Ziwa Tanganyika na nyingine Ziwa Victoria. Hata hivyo, meli hizi ni chakavu na zinahitaji matengenezo makubwa ya mara kwa

mara yanayohitaji fedha. Taasisi pia inakabiliwa na ukosefu wa fedha za kuedesha shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, hakuna taasisi ya utafiti duniani iliyofanikiwa bila kuwa na fedha za kutosha na zana zingine za utafiti. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu huo na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuisidia taasisi hii kufikia malengo yake.

(c) **Bodi ya Maziwa Tanzania (*Tanzania Diary Board - TDB*)**

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) imeundwa na kupewa uwezo na Sheria ya Maziwa (Sura 262) ya Mwaka 2004. Bodi ilizinduliwa tarehe 11 Novemba, 2005 kama Mamlaka ya Kuendeleza, Kusimamia na Kukuza Sekta ya Maziwa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Bodi imeonesha mafanikio yafuatayo: -

(i) Kupitia mafunzo ya ufugaji bora na kuhimiza teknolojia, Bodi ya Maziwa Tanzania imewezesha ongezeko la uzalishaji wa maziwa nchini kutoka lita bilioni 1.3 mwaka 2005/2006 hadi kufikia lita bilioni 3.972 mwaka 2023/2024. Aidha, idadi ya ng'ombe wa maziwa imeongezeka kutoka 434,760 mwaka 2005/2006 hadi 1,402,973 mwaka 2023/2024;

(ii) Ongezeko la ukusanyaji wa maziwa katika vituo vya kukusanyia maziwa kutoka lita milioni 38.04 katika vituo 184 mwaka 2005/2006 hadi lita milioni 93.4 katika vituo 258 mwaka 2023/2024. Aidha, hadi kufikia Juni, 2024 jumla ya wadau 7,013 wamesajiliwa na wanafanya biashara ya maziwa bora na salama;

(iii) Wizara kupitia TDB imeendelea kuwezesha viwanda vya usindikaji wa maziwa ambapo usindikaji umeongezeka kutoka lita 150,000 katika viwanda

22 mwaka 2005/2006 hadi lita milioni 81.8 katika viwanda 152 mwaka 2023/2024; na

(iv) Unywaji wa maziwa na ulaji wa mazao yatokanayo na maziwa umeongezeka kutoka lita 35 kwa mtu kwa mwaka (mwaka 2005/2006) hadi kufikia lita 67.5 kwa mtu kwa mwaka (mwaka 2023/2024).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, TDB inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha soko lisilo rasmi (uuzaji wa maziwa mitaani) linalokisiwa kuvuta zaidi ya asilimia 90 ya maziwa yanayozalishwa nchini;

(ii) Upungufu wa watumishi ambapo mahitaji halisi ni watumishi 64 lakini waliopo ni watumishi 42. Upungufu huu umechangia Bodi kutowafikia wadau wengi zaidi katika maeneo ya kanda; na

(iii) Upungufu wa fedha umechangia Bodi kushindwa kutekeleza kwa ufanisi baadhi ya shughuli zake ikiwemo ukaguzi wa wadau na kurasimisha tasnia ya maziwa.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa soko lisilo rasmi (uuzaji wa maziwa mitaani) unasababisha nchi kukosa mapato yanayotokana na uzalishaji/uuzaji wa bidhaa kiholela. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuhakikisha maziwa yote yanaingia kwenye mfumo rasmi kwa kuwasajili wafanyabiashara wote wa maziwa nchini. Aidha, Serikali iendelee kuvutia wawekezaji wa viwanda vya kuchakata maziwa na kusimamia kujenga mtandao utakaorahisisha mazao ya wafugaji kufika viwandani.

(d) **Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (*Tanzania Livestock Research Institute - TALIRI*)**

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 4 ya Mwaka 2012 na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Namba 30, Juzu 93 la tarehe 27 Julai, 2012. Majukumu ya TALIRI kwa mujibu wa Sheria ya uanzishwaji wake, ni pamoja na kufanya tafiti kuhusu uzalishaji, ukuzaji wa ufugaji wa mifugo na uendelezaji wa mifugo yenye mavuno mengi. Uendelezaji wa malisho ya mifugo, afya ya wanyama pamoja na tafiti nyingine zinazolenga kuboresha na kustawisha tasnia ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifahamishwa kuhusu mafanikio yaliyofikiwa kama ifuatavyo:-

(i) Uzalishaji wa mbari bora ya ng'ombe jamii ya Mpwapwa. Jitihada zilizofanyika kwa takribani miongo mitatu hadi mwaka 1958 zilipelekea upatikanaji wa ng'ombe mwenye asilimia 62 ya ng'ombe wa Bara Asia (*32% Red Sindhi; 30% Sahiwal*);

(ii) Uzalishaji wa mbari bora za mbuzi jamii ya Malya. Taasisi ya Utafiti wa mifugo Tanzania (TALIRI) ilifanya na kukamilisha utafiti wa mbuzi wa jamii ya Malya ambaye ana sifa ya kuwa na uzito mkubwa, maziwa mengi na amehifadhi vinasaba vya ustahimilivu wa magonjwa na mazingira magumu;

(iii) Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania imeendelea kuhifadhi kosaafu za mifugo ya asili nchini katika vituo vya TALIRI West Kilimanjaro, TALIRI Kongwa na maendeleo ya kurejesha

kosaafu ya kuku wa asili aina ya Horasi katika kituo cha TALIRI Naliendele;

(iv) Ili kuweza kufanya mabadiliko ya haraka ya kosaafu katika uzalishaji, njia za usaidizi ni muhimu ambapo kati ya hizo uhimilishaji ni jambo linalofanyiwa kazi kwa karibu na TALIRI; na

(v) TALIRI inaendeleza utafiti wa malisho bora kulingana na mabadiliko ya tabia nchi na nyanda za kiikolojia. Mpaka sasa TALIRI imefanya utafiti na kukamilisha usajili wa aina tano (5) za mbegu za malisho yanayofanya vizuri katika maeneo kadhaa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa, Taasisi hii inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha pamoja na rasilimali watu ambazo kimsingi, zinaipunguzia Taasisi hii kasi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itatenga bajeti ya kutosha pamoja na kuipatia taasisi watumishi wa kutosha ili kupata tija iliyokusudiwa katika Sekta ya Mifugo.

(e) **Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (*Fisheries Education and Training Agency - FETA*)**

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi - FETA ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iliyoanzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura Na. 245 na Marekebisho ya Mwaka 2009 (*The Executive Agencies Act Cap. 245, Revised Edition 2009*) kupitia Tamko la Serikali Na. 356 la 28/10/2011.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa majukumu ya FETA kama ifuatavyo:-

(i) FETA imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu (*long courses*) tangu ilipoanzishwa rasmi mwaka 2011 na kabla ya hapo Vyuo vya Uvuvi vya Nyegezi na Mbegani ndio vilikuwa vikitoa mafunzo ya muda mrefu;

(ii) Wakala imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi katika kozi mbalimbali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 jumla ya washiriki 4,035 walipata mafunzo, hivyo mpaka sasa jumla ya washiriki 65,698 wamehudhuria mafunzo hayo tangu Wakala ilipoanzishwa; na

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Programu ya BBT- LIFE kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya yaliyopatikana, Kamati ilifahamishwa kuwepo kwa changamoto zifuatazo:-

(i) Upungufu wa watumishi wapatao 158 kulingana na kada zilizopo kwenye Muundo;
(ii) Gharama kubwa za kuendesha Wakala (Chuo cha Uvuvi);
(iii) Uchakavu na upungufu wa miundombinu na vitendea kazi ikiwemo nyumba za watumishi, madarasa, magari, mabweni, migahawa, kumbi za mikutano, maktaba, mabwawa, vitotoleshi na maabara hususani kwenye Kampasi ya Mbegani ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na watumishi;
(iv) Uchakavu wa meli za kufundishia mafunzo ya vitendo katika Kampasi ya Mbegani;

(v) Waombaji wa mafunzo kushindwa kutuma maombi baada ya kubaini kuwa chuo hakipo miongoni mwa vyuo vya kati vinavyopata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo (HELSB);
(vi) Eneo la Kampasi ya Kibirizi - Kigoma kukumbwa na changamoto ya kujaa maji baada ya Ziwa Tanganyika kuongezeka kina; na
(vii) Kukosa wataalam wenye sifa za kitaaluma ili washiriki katika fursa za Uchumi wa Buluu katika Uvuvi wa Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zinapunguza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wakala. Kamati ina maoni kuwa Serikali iweke mikakati ya makusudi kuzitatua changamoto zote zinazoikabili ili kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(f) **Maabara ya Taifa ya Uvuvi (*National Fish Quality Control Laboratory - NFQCL*)**

Mheshimiwa Spika, Maabara ya Taifa ya Uvuvi (NFQCL) ilianzishwa Mwaka 1997 Nyegezi Mwanza kwa lengo la kudhibiti ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi nchini.

Lengo la Serikali kuanzisha maabara ni kuwa na chombo mahususi chenye jukumu la kusimamia na kuhakiki viwango vya usalama na ubora wa samaki na mazao ya uvuvi ili kulinda afya ya walaji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Maabara ya Taifa ya Uvuvi imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Kutoa huduma za uchunguzi kwa wateja wake;

(ii) Kuwa na mitambo thabiti ya upimaji na uchunguzi;

(iii) Ithibati ya maabara katika vipimo mahususi vya matakwa ya wateja wake na wataalam bingwa waliothibitishwa na bodi za ithibati katika eneo la umahiri wa uchunguzi wa maabara;

(iv) Maabara kupata vyeti vya kutambulika Kimataifa (*Accreditation Certificates*);

(v) Kuimarika kwa masoko ya samaki na mazao ya uvuvi; na

(vi) Kuongezeka kwa makusanyo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio tajwa hapo juu, Kamati ilifahamishwa uwepo wa changamoto mbalimbali zinazoikabili Maabara ya Taifa ya Uvuvi kama ifuatavyo:-

(i) Kulinda ithibati ya maabara iliyofikisha miaka zaidi ya 15 ambapo ikiwa itaondolewa inaweza kusababisha kushindwa kukidhi vigezo na matakwa ya masoko ya samaki na mazao ya uvuvi ya ndani, kikanda na kimataifa;

(ii) Kufanya manunuzi mbalimbali ya vitendanishi hususani madawa, kemikali, sampuli maalumu za kujipima umahiri (*Proficiecy Testing Samples*) na vifaa vya upimaji;

(iii) Kufanya matengenezo kinga, ugezi na kukwamua hitilafu (*Breakdown*) kwa vifaa vya maabara; na

(iv) Maabara kukosa baadhi ya mitambo na vifaa vyenye sifa inayoendana na teknolojia ya kisasa ya uchunguzi wa usalama na ubora wa samaki na mazao ya uvuvi kulingana na matakwa ya fursa za masoko mbalimbali tunayopata.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa changamoto zote hizi zinahusiana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya maabara hii. Kamati inaitaka Serikali kuipa umuhimu unaostahili maabara hii kwa kuitengea bajeti ya kutosha kukidhi mahitaji ya msingi na kuendelea kuhudumia wananchi kama ilivyokusudiwa. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa, wananchi wengi wanapata taarifa za uwepo wake ili wafikiwe na huduma zinazotolewa.

(g) **Wakala wa Maabara ya Veterinari (*Tanzania Veterinary Laboratory Agency – TVLA)***

Mheshimiwa Spika, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) ni Wakala ya Serikali chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iliyoanzishwa kwa Sheria ya Wakala za Serikali, Sura Na. 245, iliyofanyiwa marekebisho Mwaka 2009.

Wakala hii ilitokana na kuunganishwa kwa iliyokuwa Maabara Kuu ya Mifugo (CVL), Vituo vya Kanda vya Uchunguzi na Utambuzi wa Magonjwa ya Mifugo (VICs), Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo (TTRI) Tanga na Kituo cha Utafiti wa Ndorobo (TTRC) Kigoma.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzishwa kwa Wakala hii lilikuwa ni kupata chombo ambacho kitajiendesha kibiashara ili kushughulikia kwa ufanisi uboreshaji wa afya ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania katika utekelezaji wa majukumu yake, imepata mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na: -

(i) Uzalishaji wa chanjo umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka hali inayoonesha kuwa elimu ya umuhimu wa chanjo na uchanjaji wa mifugo inazidi kuenea nchini. Katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita (2019/2020 hadi 2023/2024)

jumla ya dozi 332,690,959 zilizalishwa na kusambazwa nchini;

(ii) Kuanzisha vituo vipya viwili (2) vya wafugaji kutoka maeneo mbalimbali nchini na kupata huduma na bidhaa za Wakala kupitia katika vituo vyake;

(iii) Kupatikana kwa Ithibati (*accreditation*) kwa vipimo 10 vya maabara ambapo kumetokana na Wakala kuendelea kutekeleza mfumo wa ubora wa kazi za maabara (*Laboratory Quality Management System*) na kufanikiwa kupata Ithibati (*accreditation*) ya kimataifa kwa vipimo kumi (10) vya kimaabara;

(iv) Wakala imefanikiwa kuongeza sampuli za wanyama zinazopokelewa katika maabara zake kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na utambuzi wa magonjwa kutoka sampuli 4,000 mwaka 2012 kufikia jumla ya sampuli 28,560 mwaka 2023/2024;

(v) Wakala kupitia kwa wataalamu wake imefanikiwa kushiriki katika utekelezaji wa dhana ya "Afya Moja" ambayo inawaleta pamoja wataalamu kutoka Sekta za Mifugo, Afya na Mazingira ili kutatua changamoto za magonjwa kwa binadamu. Wakala ina wawakilishi katika Kamati Maalumu inayosimamia masuala ya Afya Moja nchini; na

(vi) Wakala imefanikiwa kujengea uwezo maabara ya kupima ubora wa vyakula vya mifugo ambapo imenunua mashine za kisasa zinazoongeza ufanisi na kupunguza muda wa majibu kutoka siku sita (6) hadi siku moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika maabara hii, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi.

(i) Uchakavu wa miundombinu ya majengo, vyombo vya usafiri na vifaa vya maabara;

(ii) Upungufu wa rasilimali watu kutokana na watumishi wanaostaafu na wengine kuhamia kwenye taasisi nyingine; na

(iii) Uhaba wa vitendanishi vya maabara, kemikali na vifaa vingine vya kuzalishia chanjo;

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Wakala hii ni muhimu kwa mustakabali wa sekta ya mifugo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha ili kutatua changamoto zilizotajwa ambazo kimsingi zinasababishwa na ufinyu wa bajeti.

(h) **Bodi ya Nyama Tanzania (*Tanzania Meat Board - TMB*)**

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Nyama Tanzania imeundwa kwa Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura 421 na ilianza kufanya kazi mwaka 2008. Pamoja na mambo mengine, Bodi ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendeleza shughuli mbalimbali za uzalishaji zinazofanyika katika mnyororo wa thamani wa Tasnia ya Nyama.

Mheshimiwa Spika, Katika kuekeleza majukumu yake Bodi ya Nyama imekuwa na mafanikio yafuatayo: -

(i) Imehuisha jumla ya kazi za wadau 5,832 sawa na 83.6% ya lengo la kuhuisha kazi za wadau 6,978;

(ii) Imefanikiwa kusajili wadau wapya 1,432 sawa na 56% ya lengo la kusajili wadau wapya 2,549;

(iii) Imetoa mafunzo (SOPs) kwa wadau wa Tasnia ya Nyama wapatao 9,368 sawa na 77.5% ya lengo la kutoa mafunzo kwa wadau 12,090;

(iv) Imekagua jumla ya kazi za wadau 7,710 sawa na 85.7 % ya lengo la kukagua kazi za wadau 9,000;

(v) Kuwezesha Jumuiya ya Wafanyabiashara kutafuta fursa za masoko nje ya nchi kwa kuratibu safari kwa kampuni/viwanda vitatu vya nyama kwenda nje ya nchi kutafuta masoko;

(vi) Imefanikiwa kutoa jumla ya vibali 2,045 vya kupeleka nyama nje ya nchi sawa na tani 6,881.3 zenye thamani za Dola za Kimarekani milioni 27; na

(vii) Imeweza kuunganisha mfumo wake wa kutoa vibali (MIMIS) na mfumo jumuishi wa TRA wa utoaji wa shehena katika malango ya forodha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Bodi pia inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Ukosefu wa majengo ya ofisi (Makao Makuu pamoja na Ofisi za Kanda);

(ii) Ukosefu wa vitendea kazi hususan magari na samani;

(iii) Kuongezeka kwa mahitaji ya malighafi (mifugo bora) kwa ajili ya viwanda vya nyama; na

(iv) Uanzishwaji na uimarishaji wa vyama vya wadau wa Tasnia ya Nyama.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya changamoto zinazoikabili Bodi ya Nyama kimsingi inatokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Kamati inaitaka Serikali kuona umuhimu wa kutenga bajeti ya kutosha kwa sekta hii ili kuweza kufikia malengo ya kuinua na kuiongezea thamani sekta hii.

(i) **Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority - DSFA*)**

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority - DSFA*) ni Taasisi iliyoanzishwa rasmi Februari, 2010 chini ya Sheria ya Bahari Kuu, Sura ya 388 ya Mwaka 1998. Taasisi hii inasimamia shughuli zote za uvuvi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili Taarifa hii, Kamati ilijulishwa kuwa, Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu yake imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Kukusanya mapato ya Serikali na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni nchini ambapo jumla ya Shilingi 3,907,780,000.00 kati ya shilingi 2,295,343,400.00 zilizopangwa kukusanywa kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2024 sawa na asilimia 170 ya lengo;

(ii) Kuimarika kwa ulinzi na usalama wa shughuli za uvuvi; Ukaguzi wa meli bandarini na baharini, doria za kwenye maji na ndege, matumizi ya mifumo kwa kushirikiana na Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo Zanzibar - KMKM, Jeshi la Wanamaji - Navy, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Mifugo - Zanzibar na Wizara ya Mifugo;

(iii) Kuendelea kutekeleza makubaliano ya Kikanda na Kimataifa ya kudhibiti uvuvi haramu kwa kufanya kaguzi ya meli 12 za uvuvi wa bahari kuu;

(iv) Kutoa elimu kwa wadau zaidi ya 140 wakiwemo maafisa uvuvi, maafisa wa vikosi vya ulinzi (Marine Police, Navy, KMKM) kuhusu udhibiti wa uvuvi haramu;

(v) Kuandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Uvuvi wa Bahari Kuu na Mikakati ya Utekelezaji wake; na

(vi) Ajenda ya Utafiti wa Uvuvi wa Bahari Kuu (2020-2025), Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari, IUU NPOA, Sharks and Rays NPOA; na kuratibu tafiti za uvuvi wa jodari bahari kuu na maji ya kitaifa na ukusanyaji wa takwimu muhimu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Mamlaka hii pia inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa bahari kuu nchini;

(ii) Kutokuwepo miundombinu muhimu kwa meli za uvuvi wa bahari kuu kutia nanga nchini; na

(iii) Usimamizi na ulinzi hafifu wa rasilimali za uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudi za Serikali za kuendelea kuimarisha usimamizi wa uvuvi wa bahari kuu ikiwa ni pamoja na kujenga bandari za uvuvi. Hata hivyo, uvuvi huu muhimu bado haujapewa kipaumbele cha kutosha kwani hakuna meli za kuaminika za uvuvi kwa muda mrefu sasa. Aidha, uwekezaji katika sekta hii bado haujafikia kiwango cha kuridhisha.

SEHEMU YA TATU
3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Mtazamo na Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kutokana na Shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2024, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama yalivyoelezwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii. Kutokana na matokeo hayo Kamati ina mtazamo na maoni yafuatayo:-

(i) Upungufu wa mitaji na ufinyu wa bajeti katika miradi ya maendeleo unazorotesha utekelezaji wa miradi ya Taasisi za umma kama vile TEMDO, KMTC, SIDO, WRRB, CAMARTEC na FTC;

(ii) Mkataba wa Kuuza na Kununua Viuadudu vinavyozalishwa na NDC kupitia Kiwanda cha Biotech Products Limited – Kibaha unasuasua kutokana na TAMISEMI kutotekeleza matakwa ya Mkataba huo;

(iii) Ukosefu wa masoko ya uhakika ya vifaa na mitambo inayozalishwa nchini kutoka KMTC, TEMDO na CAMARTEC unaathiri mapato ya taasisi husika pamoja na Serikali kwa ujumla;

(iv) Suala la elimu kwa wananchi na wafugaji kuhusu ufugaji wa samaki wa vizimba ni muhimu likatekelezwa ili kuongeza ari, kipato cha mtu mmoja mmoja na Pato la Taifa kwa ujumla**;**

(v) Uwezo mdogo wa kununua (*low purchasing power*) wa wadau wa technolojia za CAMARTEC ambao ni wakulima waishio vijijini unaweza kutatuliwa kwa kuipatia CAMARTEC ruzuku ili kutimiza malengo hayo ya kupeleka zana na teknolojia rahisi vijijini;

(vi) Upungufu wa wafanyakazi pamoja na vitendea kazi unaozikabili taasisi mbalimbali za umma unachangia Taasisi hizo kutotekeleza majukumu yake ipasavyo;

(vii) Kutotekelezwa kwa Mkataba wa ununuzi wa viuadudu kati ya NDC na TAMISEMI kumepelekea deni la mtaji wa uendeshaji wa kiwanda cha Viuadudu la NSSF kuongezeka kutokana na riba;

(viii) Upungufu wa maghala ya kuhifadhia mazao hasa katika maeneo ya wakulima, umechangia mazao kuharibikia shambani kutokana na baadhi ya wakulima kushindwa kumudu gharama za usafiri;

(ix) Kutokuwepo kwa mashine za kukagulia mizigo katika vituo vya mipakani kunaweza kuikosesha Serikali mapato lakini pia kuhatarisha uingizwaji wa bidhaa zisizohitajika nchi;

(x) Upatikanaji wa sukari inayozalishwa nchini bado haujitoshelezi, jambo linalosababisha kutumia fedha za kigeni kuagiza kutoka nje ya nchi;

(xi) Kuanguka kwa bei ya mafuta ya alizeti kumesababisha wakulima wengi kuacha kulima zao hili. Hali hii inapaswa kupatiwa uvumbuzi ili kunusuru zao hili;

(xii) Tija ndogo ya Sekta ya umwagiliaji inayotokana na fedha za miradi ya umwagiliaji kutotolewa kwa wakati na kwa kiasi sahihi;

(xiii) Tasnia ya chai nchini imedorora kutokana na wawekezaji waliochukua mashamba na viwanda vya chai kushindwa kuyaendesha kwa mujibu wa Mkataba

(xiv) Kutokuwepo na mfumo endelevu na unaoeleweka wa chanjo ya mifugo kumesababisha wafugaji kukosa soko la nyama nje ya nchi;

(xv) Upungufu wa majosho na malisho ya uhakika umesababisha mifugo kudorora na wakati mwingine kufa kwa kukosa huduma;

(xvi) Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika udhibiti wa uvuvi haramu kumechangia kupunguza ufanisi wake;

(xvii) Mfuko wa Pembejeo unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti, mikopo chechefu, kutomudu gharama za ukaguzi na ufuatiliaji wa wakopaji;

(xviii) Uvamizi wa maeneo ya Hifadhi na matumizi ya zana haribifu na zisizo endelevu katika uvuvi, kunachangia uharibifu wa mazingira ya Bahari;

(xix) Sera, Sheria na Kanuni zinazotumika katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, zisipofanyiwa mapitio zitaendelea kuweka misimamo iliyopitwa na wakati, kuweka masharti yasiyoendana na hali halisi na kuweka taratibu zisizokidhi mahitaji. Aidha, Sera, Sheria na Kanuni hizo za kila Sekta zisipofungamanishwa na miongozo, masharti na taratibu za Sekta nyingine kati ya hizo zitakosesha manufaa ya kiuchumi ya Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo na Uvuvi.

3.2 Mapendekezo

3.2.1 Upungufu wa Mitaji na Bajeti ya Maendeleo kwa Taasisi na Mashirika ya Umma

KWA KUWA, Taasisi kama TEMDO, WRRB, CAMARTEC, KMTC, SIDO na FTC zinakabiliwa na upungufu wa fedha za uendeshaji pamoja na za Miradi ya Maendeleo;

NA KWA KUWA, upungufu huo unapelekea Taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake na hivyo kutofikia malengo ya kuhudumia na kuleta ustawi wa wananchi kama ilivyokusudiwa pamoja na kuikosesha Serikali mapato kwa ujumla;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini ya kina na kuzipatia taasisi zake bajeti ya kutosha ya uendeshaji na ya maendeleo ili ziweze kutoa huduma kwa ufanisi na kuongeza mapato ya Serikali.

3.2.2 Ukosefu wa Soko la Uhakika la Bidhaa Zinazozalishwa Nchini

KWA KUWA, hali ya jumla ya upatikanaji wa masoko ya uhakika hasa kwa bidhaa zinazozalishwa na Taasisi kama vile TEMDO na CAMARTEC hairidhishi kutokana na:-

(i) Taasisi za Serikali kutokuwa na utayari wa kununua bidhaa husika hata kama zina ubora unaokubalika kutokana na taratibu za manunuzi;

(ii) Bidhaa zinazozalishwa kuwa ghali hivyo wanunuzi kutokuwa na uwezo wao wa kununua; mfano mdogo ni CAMARTEC ambapo wanunuzi wa bidhaa ni wakulima wa vijijini ambao uwezo wa kununua uko chini;

NA KWA KUWA, ukosefu huo wa masoko unapelekea:-

(i) Taasisi kushindwa kuuza bidhaa na hivyo kujiendesha kwa hasara pamoja na kuikosesha Serikali mapato; na

(ii) Serikali kutumia fedha nyingi za kigeni kununua bidhaa nje ya nchi ambazo zinapatikana nchini.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia yafuatayo:-

(i) Serikali iweke utaratibu mahsusi wa manunuzi utakaowezesha bidhaa zinazopatikana ndani ya nchi zitumike ili kuinua na kukuza wazalishaji wa ndani na kuokoa fedha za kigeni; na

(ii) Serikali izipatie ruzuku Taasisi hasa zinazopeleka huduma kwa wananchi moja kwa moja kama vile CAMARTEC na SIDO ili kuwapatia unafuu wananchi wanaonunua bidhaa hasa zana za kilimo.

3.2.3 Mfumo wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)

KWA KUWA, changamoto ya uchache wa maghala na baadhi kuwa mbali na maeneo ya mashamba hulazimisha wakulima kusafiri umbali mrefu kupeleka mazao;

NA KWA KUWA; hali hiyo imesababisha mambo yafuatayo:-

(i) Wakulima kuingia gharama kubwa kusafirisha mazao umbali mrefu; na

(ii) Madalali hutumia fursa hiyo kununua mazao kutoka kwa wakulima kwa bei ndogo na hivyo kukwamisha utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi za ghala;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iongeze kasi ya kushirikiana na Sekta Binafsi kujenga maghala ya kutosha katika maeneo ya wakulima;

(ii) Serikali ijumuishe mazao ambayo bado hayajaingizwa kwenye mfumo wa stakabadhi za ghala ikiwemo kahawa ili kunufaisha wakulima wengi zaidi;

(iii) Serikali iweke mfumo mzuri wa uendeshaji na usimamizi wa maghala ili kudhibiti tabia za wamiliki wa maghala kuwalipisha wakulima gharama zisizowahusu; na

(iv) Serikali itoe elimu kwa wakulima kuhusu umuhimu wa kuuza mazao yao kwa kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala.

3.2.4 Hali ya mafuta ya kula nchini

KWA KUWA, bado tunakabiliwa na upungufu wa mafuta ya kula unaosababishwa na wakulima wengi kusitisha kilimo cha alizeti kutokana na kukosa soko la uhakika;

NA KWA KUWA, upungufu huo wa mafuta unasababisha wafanyabiashara kuingiza shehena kutoka nje ambayo huuzwa kwa bei ya juu;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iendelee kuhamasisha, kuendeleza na kujenga viwanda vya kutosha vya kuzalisha mafuta ya kula nchini ili kupunguza utegemezi wa uingizaji wa mafuta ya kula na kujihakikishia usalama wa chakula nchini;

(ii) Serikali iendelee kupitia upya vivutio ilivyotoa kwa wazalishaji wa ndani wa mafuta ili kuondoa athari zilizojitokeza kwa wakulima wa alizeti; na

(iii) Alizeti kama ilivyo kwa mazao mengine, iwekewe bei ambazo zitawavutia wakulima ili wahamasike kulima kwa wingi.

3.2.5 Upatikanaji wa Sukari Nchini

KWA KUWA, upatikanaji wa sukari inayozalishwa nchini bado haujitoshelezi, jambo linalosababisha kuagiza kutoka nje ya nchi ili kuziba nakisi;

NA KWA KUWA, kutopatikana kwa sukari ya kutosha kunaweza kusababisha:-

(i) Upungufu wa sukari;
(ii) Kutowafikia walaji kwa wakati; na
(iii) Bei kuwa juu;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya sukari ili kuongeza uzalishaji.

3.2.6 Mkataba wa Ununuzi wa Viuadudu kati ya NDC na TAMISEMI

KWA KUWA, Mkataba wa Kuuza na Kununua Viuadudu vinavyozalishwa na NDC kupitia Kiwanda cha Biotech Products Limited – Kibaha unasuasua kutokana na TAMISEMI kutotekeleza matakwa ya Mkataba huo;

NA KWA KUWA, kutokelezwa kwa Mkataba huo kumepelekea mambo yafuatayo:-

(i) Deni la Mtaji wa uendeshaji wa Kiwanda cha Viuadudu la NSSF kuongezeka kutokana na riba; na

(ii) Mpango wa kutokomeza malaria kuendelea kusuasua na malengo ya uanzishwaji wa kiwanda kutotimia;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali itoe tamko la kuhuisha na kutekeleza Mkataba huu kikamilifu ili kukiwezesha kiwanda kufanya kazi kwa tija na kulipa madeni; na

(ii) Viuatilifu vya mazao vizalishwe ili kupunguza ombwe la mahitaji ya viuatilifu nchini.

3.2.7 Upungufu wa Scanners Katika Mipaka Nchini

KWA KUWA, baadhi ya vituo vya mipakani vinakabiliwa na ukosefu wa scanners;

NA KWA KUWA, ukosefu huo unaweza kusababisha yafuatayo:-

(i) Kuikosesha Serikali mapato kutokana na wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia mwanya huo kukwepa kodi;

(ii) Mizigo kukaa mipakani kwa muda mrefu na baadhi yake kuharibika; na

(iii) Uingizwaji wa bidhaa zisizohitajika nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua za haraka na za makusudi ili kuhakikisha inaweka mifumo imara ya udhibiti wa uingizaji wa bidhaa nchini katika maeneo yote ya mipakani ikiwa ni pamoja na kufunga scanners.

3.2.8 Sekta ya Biashara Nchini

KWA KUWA, Sekta ya Biashara ina mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi, uongezaji wa pato la Taifa na kodi zinazotokana na wafanyabiashara;

NA KWA KUWA, Sekta hii inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na Sera, Sheria na baadhi ya Kanuni kupitwa na wakati na hivyo kuathiri wafanyabiashara wakubwa na wadogo pamoja na pato la Taifa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha vikwazo na changamoto hizo zinaondolewa ikiwa ni pamoja na kufanyia mapitio Sera na Sheria zinazohusika ili kuimarisha Sekta ya Biashara nchini.

3.2.9 Ujenzi wa Viwanda Nchini

KWA KUWA, nchi inakabiliwa na upungufu wa viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali;

NA KWA KUWA, ukosefu wa viwanda hivyo unasababisha:-

(i) Uingizwaji wa bidhaa kutoka nje kwa kutumia fedha za kigeni;

(ii) Ukosefu wa ajira kwa vijana;

(iii) Kukosekana kwa soko la malighafi inayozalishwa hapa nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuhamasisha na kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji wa viwanda ili kupunguza changamoto ya ajira inayoendelea kukua siku hadi siku, kuagiza bidhaa kutoka nje na kuongeza soko la malighafi ambalo litaongeza mapato ya Taifa na mwananchi mmoja mmoja.

3.2.10 Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (Ward *Agricultural Resources Centres*)

KWA KUWA, Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata katika maeneo mbalimbali nchini vilivyokabidhiwa Halmashauri za Wilaya kwa lengo la kuwafikishia wakulima huduma mbalimbali ikiwemo elimu na huduma za ugani havitekelezi azma hiyo kutokana na baadhi kubadilishiwa matumizi kinyume na utaratibu;

NA KWA KUWA, kubadilishwa matumizi kumepelekea kutofikiwa kwa malengo ya kupeleka huduma za kuridhisha za ugani pamoja elimu katika ngazi hiyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Iviondoe vituo hivyo kwenye usimamizi wa Halmashauri na vikabidhiwe Wizara ya Kilimo ili viwe *mechanization centers* vitakavyosimamiwa na Wakala wa Wagani itakayoanzishwa;

(ii) Uanzishwaji wa Wakala wa Wagani ambao uko katika hatua za mwanzo uharakishwe ili vituo hivyo vilete tija iliyokusudiwa;

(iii) Serikali itenge fedha za kutosha kununua matrekta angalau mia moja kwa kuanzia ili vituo hivyo viweze kufanya kazi kwa ufanisi;

(iv) Miundombinu ya Vituo kama maji, umeme na barabara viboreshwe ili vituo vifikike kwa urahisi; na

(v) Vituo vyote vipatiwe hati za umiliki na kuwekewa uzio ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima.

3.2.11 Mchango mdogo wa Tasnia ya Umwagiliaji katika Sekta ya Kilimo

KWA KUWA, Tasnia ya Umwagiliaji imebainika kuwa na mchango mdogo katika Sekta ya Kilimo kutokana na:-

(i) Ucheleweshaji wa fedha toka Hazina kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

(ii) Idadi ndogo ya Wataalamu mbalimbali wa Umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya; na

(iii) Mwamko mdogo wa wakulima katika kulipia ada za huduma za umwagiliaji

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinakwamisha tija iliyokusudiwa na kusababisha uzalishaji mdogo wa sekta ya kilimo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ifanye uchambuzi wa kina kubaini Miradi yote inayohusiana na ujenzi wa mabwawa na kilimo cha umwagiliaji ili utekelezaji wake uwe na tija kwa Sekta hii muhimu ya Kilimo. Aidha, kutokana na wingi wa Miradi na kwa kuzingatia ufinyu wa bajeti, Serikali iainishe vipaumbele vya Miradi ya kutekelezwa na itengewe bajeti kwa ajili ya utekelezaji;

(ii) Serikali iendelee kuongeza na kutoa kwa wakati fedha za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji; na

(iii) Serikali iweke mifumo mizuri itakayowawezesha wakulima kulipa ada za huduma kwa wakati. Aidha, mifumo ya ufuatiliaji wa madeni yatokanayo na ada hizo iimarishwe.

3.2.12 Tasnia ya Chai Nchini

KWA KUWA, wawekezaji waliochukua mashamba na viwanda vya chai wameshindwa kuyaendesha kwa mujibu wa Mkataba;

NA KWA KUWA, kutokuendelezwa huko kumepelekea yafuatayo:-

(i) Tasnia ya chai kudorora;

(ii) Uingizwaji wa chai toka nje ya nchi; na

(iii) Wakulima wadogo wa chai kuendelea kuwa na hali duni ya maisha kutokana na kutolipwa fedha za mauzo ya chai yao;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ikamilishe haraka majadiliano na Wawekezaji wa viwanda ambao wameshindwa kuendesha mashamba na viwanda kwa lengo la kuwapa wawekezaji wengine wenye uwezo. Aidha, Serikali ipitie upya mfumo wa uendeshaji wa mashamba na viwanda hivyo kwa nia ya kuwahusisha wakulima wadogo na wakati kwenye uendeshaji na umiliki.

3.2.13 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)

KWA KUWA, Wakala unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ufinyu wa bajeti; na

(ii) Bajeti inayoidhinishwa na Bunge haitoki kwa wakati;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinasababisha Wakala kushindwa kununua mazao kwa wakati kutoka kwa wakulima;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iiongezee Wakala bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoidhinishwa zinatoka kwa wakati. Vilevile iwezeshwe kununua, kutunza na kusambaza sukari uhaba unapotokea.

3.2.14 Mfuko wa Pembejeo za Kilimo

KWA KUWA, Mfuko wa Pembejeo unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti, mikopo chechefu, kutomudu gharama za ukaguzi na ufuatiliaji wa wakopaji;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinachangia kutopatikana kwa pembejeo kwa wakati;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha watu wote wanaodaiwa na AGITF wanalipa madeni yao. Aidha, Serikali ifute mikopo isiyolipika kwa mujibu wa Sheria za Fedha;

(ii) Serikali ianzishe Ofisi za Kanda ili kurahisisha usimamizi, ufuatiliaji na kusaidia utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa wakati;

(iii) Serikali ihakikishe AGITF inaweka mfumo wa mikopo yenye riba nafuu ambayo wakulima wanaweza kumudu.

3.2.15 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB)

KWA KUWA CPB inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) mtaji usiotosheleza (*insufficient working capital*);
(ii) Sheria ya uendeshaji ambayo haiipi Bodi uwezo na urahisi wa kushindana kibiashara;
(iii) Muundo wa CPB kutoendana na majukumu yake;
(iv) Sheria ya Manunuzi; na
(v) Ajira zenye ukomo wa miaka miwili.

NA KWA KUWA changamoto hizo zinapelekea Bodi kutotekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kupoteza wafanyakazi wengi ambao wamekwisha jengewa uwezo;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuchukua hatua madhubuti kuiongezea nguvu CPB ili iweze kutengeneza soko la uhakika kwa wakulima. Aidha, Serikali iharakishe hatua zinazoendelea za kuifanya taasisi hii kuwa kampuni ili iweze kufanya kazi zake kibiashara na kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

3.2.16 Chanjo ya Mifugo

KWA KUWA mfumo wa chanjo za mifugo haujapata msukumo unaostahili ikiwa ni pamoja na kutokuwepo mifumo endelevu katika ngazi zote inayoeleweka vizuri kwa wafugaji;

NA KWA KUWA, kukosekana huko kwa mfumo kunaikosesha Serikali fedha za kigeni na wafugaji kutonufaika na mifugo yao;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ikamilishe mchakato wa kutoa chanjo kwa mifugo yote nchini;

(ii) Serikali itoe Elimu kwa wananchi ili watambue umuhimu wa chanjo kwa mifugo yao;

(iii) Maafisa ugani wapewe elimu ya namna ya kuchanja ili kutosababisha madhara kwenye mifugo; na

(iv) Serikali itoe bei elekezi ya chanjo kwa kila aina ya mifugo ili kudhibiti upandishwaji holela wa gharama za chanjo.

3.2.17 Majosho na malisho ya mifugo

KWA KUWA, kuna upungufu mkubwa wa majosho, mabwawa na malisho ya mifugo;

NA KWA KUWA, upungufu huo unasababisha kupata mazao duni ya mifugo ikiwa ni pamoja na kuugua na hata kufa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ihakikishe inaongeza bajeti ya kujenga majosho, mabwawa na malisho ya kutosha na yanayofaa kwa matumizi ya mifugo;

(ii) Serikali iharakishe ukamilishaji wa uanzishwaji wa Mamalaka ya Mifugo itakayosimamia masuala ya uendelezaji wa mifugo nchini; na

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wafugaji ili waone umuhimu wa kupeleka mifugo yao kwenye majosho.

3.2.18 Uvuvi wa Vizimba

KWA KUWA, uvuvi wa vizimba haujatiliwa mkazo ipasavyo na hivyo kusababisha uhaba wa samaki katika maeneo mengi yenye vyanzo vya uzalishaji wa samaki;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa samaki kunaathiri upatikanaji wa lishe na mapato yatokanayo na soko la samaki;

KWA HIYO BASI, Serikali iendelee kuhamasisha ufugaji wa vizimba katika maeneo yote nchini ili kuhakikisha samaki wanapatikana wakati wote.

3.2.19 Udhibiti wa Uvuvi Haramu

KWA KUWA, uvuvi haramu umechangia kwa kiasi kikubwa kuharibu mazalia ya samaki na kuchangia utoroshwaji wa samaki nje ya nchi;

NA KWA KUWA hali hiyo imeathiri upatikanaji wa samaki hasa katika maeneo yote ya maziwa na bahari;

KWA HIYO BASI, Serikali iendelee kuimarisha mifumo ya udhibiti wa uvuvi haramu ili rasilimali za uvuvi ziweze kuwa na tija kwa Taifa.

3.2.20 Taasisi za Utafiti

KWA KUWA, Taasisi za Utafiti zinazosimamiwa na Sekta za Viwanda (TIRDO na TEMDO), Kilimo (TARI), Mifugo na Uvuvi (TALIRI, TVLA na TAFIRI) zinakabiliwa na ufinyu wa bajeti;

NA KWA KUWA, upungufu huo wa bajeti unasababisha yafuatayo: -

(i) Matokeo ya tafiti kuchukua muda mrefu;

(ii) Uchakavu wa miundombinu unaopunguza tija;

(iii) Kukosekana vifaa vya kutosha vya utafiti;

(iv) Upungufu wa rasiliamali watu; na

(v) Uzalishaji kutofikia lengo.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha Taasisi hizi muhimu zinatengewa bajeti ya kutosha na kuipeleka kwa wakati ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kufanya tafiti zenye manufaa katika sekta husika.

4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA

4.1 Hitimisho

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako. Mafanikio ya Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2024 hadi Januari, 2025 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali.

Ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii, unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Deodatus Mwanyika, Mb, - Mwenyekiti
2. Mhe. Mariam Mzuzuri, Mb, Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb,
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb
5. Mhe. Prof. Sospeter Mujarubi Muhongo, Mb
6. Mhe Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb

10. Mhe. Dkt. Medad Matogolo Kalemani, Mb
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
14. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb
17. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb
18. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb
19. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb
20. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
21. Mhe. Toufiq Salim Turky, Mb
22. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Mb
23. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb
24. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Selemani Said Jafo (Mb), na Naibu wake Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe, (Mb), Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb) na Naibu wake Mhe. David Ernest Silinde, (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mb, na Naibu Waziri wake Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka I.

Leonard, kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo, na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja:

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.



Deodatus Philip Mwanyika, Mb
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO

6 Februari, 2025